




## MIAKA 2 IKULU
Karipio lake kwa mawaziri na anakolenga Samia kiuchumi

UKURASA 4





# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

Jumapili Machi 5, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. 0581240

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


UKURASA 9

## CCM yashtuka tozo za mazao halmashauri

UK. 2

# Kauli ya Lema bodaboda yatikisa

UKURASA 3





Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akikagua mradi wa ujenzi wa soko la kisasa Chuini, Wilaya ya Magharibi "A" Unguja, linalojengwa na Kikosi cha Zimamoto na Uokoaji Zanzibar, alipofanya ziara ya kushtukiza jana. **PICHA: IKULU**

## Zitto: Hatutorudi nyuma kufichua uovu serikalini

UK 3


SPECIAL SUPPLEMENT

WOMEN'S DAY 8th March

The Guardian Nipashe



The Guardian Limited will publish a special supplement with **"The Guardian"** and **"Nipashe"** Newspapers, with a special report focusing on the **Women's Day** theme

**Embrace Equity**

We wish to invite you to be a part of this special supplement by publishing your **Special features, Advetorials** and **Advertisements.**

**TO BOOK YOUR SPACE PLEASE CALL US TODAY ON +255 677 020 701**

Email: advertise@guardian.co.tz or Visit us at The Guardian Limited, Mikocheni Light Industrial Area, Opposite ITV / Radio One, Dar es Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com



**MICHEZO** SIMBA KAZI MOJA TU KWA VIPERS UK. 24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Mufti na Shehe Mkuu wa Tanzania, Abubakar bin Zubeir (katikati), akizindua kitabu kijulikanacho silaha zaidi ya 40 za Muumini, jijini Dar es Salaam jana, kinachofundisha imani ya dini ya Kiislam kilichoandikwa na Mkurugenzi Taasisi ya Al-Hikma Shehe Nurdin Kishik, katika hafla ya uzinduzi wa maandalizi ya mashindano makubwa ya Qur' aan, Afrika yanayotarajiwa kufanyika Aprili 9 mwaka huu katika Uwanja wa Uhuru. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Afungwa jela maisha kwa ubakaji, ulawiti

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Singida, imemhukumu kifungo cha maisha jela mkazi wa Manispaa ya Singida, Fabiano Darabe (50) baada ya kumtia hatiani kwa makosa matano ya kubaka na kulawiti.

Hakimu Mkazi Robert Oguda, akitoa hukumu hiyo juzi, alisema vitendo vya ubakaji wa watoto chini ya miaka 10 adhabu yake ni kifungo cha maisha na kuanzia miaka 11 adhabu yake ni kifungo cha miaka 30 jela.

Hakimu Oguda alisema kwa kosa la kwanza na la tatu, mtuhumiwa atakwenda kutumikia adhabu ya miaka 30 jela kwa kila kosa na kwamba kwa kosa la pili, la nne na la tano, mtuhumiwa atatumikia adhabu ya kifungo cha maisha jela.

Pamoja na kuainisha adhabu hizo, Hakimu aliweka bayana kwamba kwa ujumla, adhabu za makosa hayo yote yatakwenda kwa pamoja, hivyo mshtakiwa atatumikia adhabu ya kifungo cha maisha jela. Kabla ya hukumu kutolewa, mshtakiwa alipewa nafasi ya kujitetea na kuiomba mahakama kumpunguzia adhabu kwa sababu ana matatizo ya kiafya.

"Lakini Mheshimiwa Hakimu, acha tu nikafie huko huko tu si wameamua kunileta huku kwa kosa ambalo sikulitenda kabisa mimi mwenyewe?" alisikika akiiomba mahakama kwa sauti ya chini huku akimtazama hakimu kabla ya kutoa hukumu yake.

Awali, Mwanasheria wa Serikali, Nuru Chiwalo, alidai kwamba mtuhumiwa alitenda makosa mawili ya ubakaji na matatu ya ulawiti kwa watoto wenye umri wa kati ya miaka mitano na miaka 11 katika Manispaa ya Singida kati ya mwaka 2018 na 2021.

"Mtuhumiwa alitenda kosa la kubaka mwanafunzi wa darasa la tano mwenye umri wa miaka 11 na kumlawiti mwanafunzi wa darasa la pili mwenye umri wa miaka saba. Vile vile alimlawiti mwanafunzi wa darasa la kwanza wakati akijua wazi kuwa kutenda kosa hilo ni kinyume cha sheria za nchi," alidai.

Kwa mujibu wa Chiwalo, serikali iliwasilisha mashahidi wanane ambao walitoa ushahidi wa vielelezo ikiwemo PF3, mlinzi wa amani, Deodatus Patrick na daktari ambaye alithibitisha kwamba watoto hao walifanyiwa vitendo vya ukatili.

Hata hivyo, kabla ya Hakimu kumtia hatiani, mwanasheria huyo alidai kwamba matukio ya ubakaji na ulawiti katika mkoa wa Singida yamekithiri na kwamba vitendo hivyo vinasababisha watu kuwa mashoga.

Pamoja na madai hayo, Chiwalo alidai kuwa mahakama hiyo haina kumbukumbu za makosa mengine ya nyuma ya mtuhumiwa huyo lakini aliiomba mahakama kuangalia sheria inasema nini kwa wakosaji wa makosa ya aina hiyo kwa kuwa kitendo cha mtoto kuingiliwa kinazuia mtoto huyo kupata haja kubwa.

"Adhabu utakayotoa ilenge kutoa elimu kwa jamii kuachana na tabia ya kuwabaka au kuwalawiti watoto wadogo na adhabu hiyo iwe fundisho kwa wazazi na walezi wengine ambao bado hawajajulikana kuwa wanajihusisha na vitendo vya aina hii," alisisitiza.

Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building-Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email: info@victoriafinance.co.tz
Website: www.victoriafinance.co.tz

## TANGAZO LA MINADA YA HADHARA

**VICTORIA FINANCE PLC** INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA WA WATANZANIA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| NA | JINA LA MDAIWA | DHAMANA | AINA NA SEHEMU YA DHAMANA | DALALI | TAREHE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | MOSSES ANDREW ODUNGA AS AN ADMISTRATOR OF THE ESTATES OF THE LATE ANDREW JUMA ODUNGA | NYUMBA | HATI MILIKI - NJIRO ARUSHA | J & J RECOVERIES | 20-03-2023 |
| 2 | HELLENA RICHARD MOSHA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KIMARA BUCHA | J & J RECOVERIES | 20-03-2023 |
| 3 | SAID JUMA TAMAMBELE | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – MAKURUMLA KAGERA | J & J RECOVERIES | 20-03-2023 |
| 4 | AMANI MUSSA MTULI | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – NZASA A,KILUNGULE DAR ES SALAAM | DIAMOND CREDIT RECOVERY CO. LIMITED | 20-03-2023 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika ofisi za wakuu wa wilaya wanaohusika.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.

217309401

# CCM yazionya halmashauri kuvizia ushuru wa mazao

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo amezionya halmashauri dhidi ya tabia ya kuvizia kila kinachosafirishwa husuani mazao ya kilimo kwa lengo la kutoza ushuru na badala yake wabuni vyanzo vya mapato na kuwa sehemu ya uwekezaji.

Akizungumza jana baada ya kukitembelea kiwanda cha kukamua mafuta cha Singida Fresh Oil Mill kilichopo mjini Singida katika mwendelezo wa ziara yake mkoani hapa, Chongolo alisema "hatuwezi kuwa na halmashauri zinazovizia kila kinachopita kwao wakichukue, kwani jambo hilo linaweza kusababisha maeneo mengine yashindwe kupelekewa bidhaa.

"Hebu fikiria mtu atoke na samaki wake mjini Mwanza afike Misungwi achajiwe, apite Kishapu achajiwe, aje Shinyanga achajiwe, aje Nzega achajiwe, aje Igunga achajiwe, apite Iramba, Mkalama na Singida achajiwe, afike Ikungi hadi Manyoni achajiwe. Sasa bidhaa hiyo hadi ifikishwe Dar es Salaam itauzwa kwa shilingi ngapi?" alihoji.

Chongolo alisema hali hiyo inakuwa hivyo kwa sababu kila halmashauri inashindwa kubuni mfumo na uwekezaji wa kwao na hivyo kutaka kuibukia na kutengeneza sheria ndogo zenye lengo la kuwaumiza wengine, jambo ambalo CCM haikubaliani nalo.

Alisema ni lazima mamlaka zinazohusika ziweke mifumo na sheria ndogo ambazo zitakwenda kusimamia ukusanyaji wa mapato katika halmashauri na kwamba sheria hiyo ziwekwe wazi kwenye mazao yanayozalishwa kwenye eneo husika ili kudhibiti kudai ushuru katika kila eneo mazao yanapopita.

Hatua ya Katibu Mkuu wa CCM kutoa onyo hilo ilitokana na kauli ya Mkurugenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya kula ya alizeti, Singida Fresh Oil Mill, Khalid Ally Omary, maarufu Shulu, aliyeeleza kuwa changamoto zimekuwa kero katika uendeshaji wa kazi ni kuwapo kwa vizuizi vingi wakati wa usafirishaji wa bidhaa za mazao ya kilimo kwenye barabara kuu.

"Kusafirisha mashudu ya alizeti kutoka Singida kwenda Kenya utapitia Singida, Oldonyosambu na Longido, unatozwa ushuru kila eneo kwa bidhaa hiyo wakati jirani zetu Uganda hawana tozo yoyote ya bidhaa hiyo wakipeleka Kenya, hali hii inasababisha ugumu kushindana na Waganda ambao tunategemea soko moja Kenya," alisema.

Ally alitaja changamoto nyingine kuwa ni kukatika kwa umeme kila mara na kusababisha uharibigu wa mashine, ubovu wa barabara na uhaba wa alizeti.

Mkurugenzi huyo alisema kwa sasa kiwanda hicho kina uwezo wa kukamua tani 90 kwa siku za alizeti na kupata lita 23,300 za alizeti lakini kutokana na ukosefu wa alizeti ya kutosha kinakamua tani 22 tu na kupata mafuta lita 6,600 kwa siku.

## HABARI KITAIFA



Mkuu wa Polisi Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, SSP Hadija Sokolo (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi Muheza, SP Kuruthumu Bambe, wakati wa kugawa msaada wa vyakula na vitu mbalimbali kwa watoto wenye mahitaji maalum, wanaosoma Shule ya Msingi Mbaramo jana, vilivyotolewa na umoja wa askari polisi wanawake mkoa huo, kuelekea maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kauli ya Lema bodaboda yatikisa

**Na Waandishi Wetu**

KAULI ya Mbunge wa zamani wa Arusha Mjini, Godbless Lema (CHADEMA), kuhusu waendesha bodaboda kwamba ni laana, imezidi kutikisa anga za siasa huku baadhi ya wabunge wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wakimpinga.

Wakati wabunge hao wakiibua mashambulizi dhidi yake, Lema jana alizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha na kutoa ufafanuzi juu ya kauli yake hiyo akibainisha kuwa biashara hiyo ni chanzo cha ulemavu na maradhi kwa vijana hao hasa kifua.

Lema alitoa kauli hiyo mapema wiki hii alipokuwa akihutubia mkutano jijini Arusha, muda mfupi baada ya kutua nchini kutoka Canada alikokuwa uhamishoni kwa takribani miaka miwili.

Katika mkutano huo, Lema alitamka: "Bodaboda, wakati ninyi mnanipokea kwa shangwe, mimi nilikuwa ninahuzunika. Bodaboda si ajira ni umaskini unaopitiliza. Hiyo ni ajira ya laana, ikemeeni. Hamwezi kufanya ajira kwa kukimbiza upepo Sh. 7,000 kwa siku. Hapana."

Kutokana na kauli hiyo, Wabunge wa CCM mkoani Singida, wakizungumza katika mkutano wa hadhara wa Katibu Mkuu wa chama hicho, Daniel Chongolo, walisema Lema amewakosea vijana waendesha bodaboda.

Mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu, alisema CCM inathamini mchango wa bodaboda katika maendeleo ya uchumi na si ajira ya laana kama alivyosema Lema. Alisema amefanya takwimu nchi ya India ambayo ina uchumi mkubwa ina waendesha bodaboda wasiopungua milioni 34.

"Kuna nchi nyingi zinaongoza kwa kuwa na waendesha bodaboda, hii ni kazi ya heshima na inarahisisha usafiri wa watu kujenga uchumi wa nchi. Kitendo cha mwanasiasa huyo kuwatukana bodaboda katika taifa letu kwamba wamelaaniwa hatuwezi kuacha bila kujibiwa kwenye majukwaa ya kisiasa," alisema.

Kingu aliwahimiza bodaboda kufanya kazi kwa kuwa CCM inawaheshimu na itaanzisha mikakati ya kuwasaidia ili kuchochea maendeleo ya kiuchumi.

**LEMA AJIBU**

Lema jana alizungumza na waandishi wa habari kuhusu mambo mbalimbali ikiwamo kutoa ufafanuzi kuhusu kauli yake hiyo ya Bodaboda.

Alisema: "Bodaboda ni ulemavu mnajitengenezea vijana kama si kuugua kifua ni kupata ajali za barabarani. Serikali inatakiwa itengeneze mfumo mzuri wa ajira na siyo bodaboda kwa vijana ,ajira zipo za aina nyingi.

"Nikiwa Canada niliona ajali ilivyowaburuza vijana zaidi ya wana pale Meru (Momela) kwenye msafara wa watu waliokuja kunipokea, kuna kijana kalazwa Nkoaranga hospitalini baada ya kuvunjika bega akiwa anaendesha bodaboda. Huu ndio umasikini ninaousemea mimi.

"Huu si usafiri wa public (umma) ndiyo maana serikali haijatengeneza bima kwa ajili ya waendesha bodaboda. Serikali inapaswa kuja na mkakati wa kuwasaidia wananchi wake na siyo kubariki uendeshaji wa bodaboda hata walikotengeneza hizi pikipiki hawazitumii maana hazitambuliki kama usafiri wa umma."

**MAAGIZO YA CHONGOLO**

Chama Cha Mapinduzi (CCM), kimetoa maelekezo mahsusi manne kwa serikali baada ya kubaini kero mbalimbali zinazowakabili wananchi kwenye sekta za afya, elimu na kilimo.

Akizungumza jana kwenye mkutano wa hadhara wilayani Singida ikiwa ni hitimisho la ziara ya siku tano ya sekretarieti ya chama hicho, Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo, alielekeza hospitali za wilaya zinazojengwa ambazo miundombinu imekamilika, zianze kutoa huduma kwa wananchi ili kudhibiti vifo vya mama na watoto.

"Ninakwenda kukutana na wahusika wa Wizara ya Afya ili kuhakikisha vifaa tiba vyote vinavyopaswa kuletwa kwenye hospitali hizo vinaletwa haraka ili tiba za msingi zikiwamo upasuaji kwa wajawazito zianze kutolewa," alisema.

Aidha, alisema CCM inaelekeza na kuweka msukumo wa kuhakikisha wahudumu wa afya wanapelekwa kwa idadi ya kutosha ili huduma zitolewe kwenye hospitali na kuleta matokeo halisi yaliyokusudiwa ya kusogeza huduma kwa wananchi.

Kuhusu elimu, alisema serikali imeweka nguvu kubwa kwenye miundombinu ya sekta hiyo na kutaka sasa ielekezwe kwenye ujenzi wa shule za kidato cha tano na sita.

Aliwahakikishia kuisukuma serikali na kuwajibika kupeleka pembejeo za mbolea ya ruzuku kwenye maeneo yaliyo karibu na wakulima katika vifungashio tofauti vidogo tofauti na sasa ambapo kuna mifuko yenye ujazo wa kilo 50.

"Tunaelekeza serikali kuanzia msimu ujao ihakikishie inaleta mbolea kwenye vifungashio tofauti kilo 10, 25 na 50 ili mwananchi yeyote anunue kwa kiwango chenye uhitaji. Hatuwezi kuwa na uwezo wa kufunga sukari nusu kilo, kilo moja hatuwezi kushindwa kufunga mbolea kwa ujazo huo," alisema.

Sekretarieti ya CCM inayoongozwa na Chongolo ilifanya ziara mkoani Singida kwa lengo la kusikiliza wananchi kujua kero zinazowakabili ambazo zinakwamisha maendeleo yao, kuhimiza uhai wa CCM na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya 2020-2025.

Chongolo na ujumbe wake waliingia jana mkoani Manyara kuendelea na ziara hiyo.

* **Imeandikwa na Augusta Njoji, SINGIDA na Tumaini Mafie, ARUSHA.**

# Zitto: Hatutorudi nyuma kufichua uovu serikalini

**Na Romana Mallya**

KIONGOZI wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe amesema hawakuingia serikalini ili kujenga serikali ambayo haiheshimu sheria za nchi, bali inayowajibika kwa watu.

Kwa kuzingatia hilo, Zitto amesema hawatoacha kusema wanapoona maslahi ya wananchi yanakanyagwa.

Alitoa kauli hiyo jana kwenye mkutano wa chama uliofanyika kisiwani Pemba kwenye Uwanja wa Tibirinzi ambako pia waliwapokea wanachama wapya 305 kutoka Chama cha Wananchi (CUF), 10 kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) na mmoja toka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Zitto alisema kwamba chama, licha ya alichokiita madhila yaliyotokea mwaka 2020, waliamua kuingia kwenye Serikali ya Umoja wa Kitaifa ili kujenga serikali inayowajibika kwa watu.

"Hatukuingia kwenye serikali ili kujenga serikali ambayo haiheshimu sheria za nchi, serikali ya namna hiyo sio serikali ambayo tunaweza kuendelea nayo. Tunataka serikali inayowajibika kwa watu.

"Na sisi kama chama ambacho tumo ndani ya serikali hiyo, ni lazima tuhakikishe uwajibikaji. Tunapoibua masuala ya watu, maslahi yetu ni watu. Bahati mbaya sana baadhi ya viongozi kwa kuwa wao uongozi ni maslahi yao, wanadhani kila mtu mwingine uongozi unaangalia maslahi yake.

"Sio sisi ACT-Wazalendo. Sisi uongozi ni maslahi ya watu, mtu ambaye anaweza akathubutu kwenda kusema kwamba 'hao ACT wanaibua hili na hili, watangaze kwanza maslahi yao', tunatangaza maslahi yetu ni Wazanzibar, hatutoacha kusema tunapoona maslahi yanakanyagwa," alisisitiza.

Alisema wataendelea kuwasemea wananchi mpaka wapate Zanzibar mpya, Zanzibar moja na yenye mamlaka kamili.

Zitto pia alikumbusha maneno ambayo Maalim Seif Shariff Hamad (hayati) aliwahi kuyasema kwenye uwanja huo mwezi Desemba mwaka 1987, kwamba "Nipo nanyi sasa hivi, ninawaahidi nitakuwa nanyi nikiwa ndani ya serikali au nje ya serikali, ninawaahidi nitakuwa nanyi nikiwa ndani ya chama au nje ya chama."

Zitto alisema jambo la msingi Maalim aliwaahidi Wazanzibar kwamba atakuwa nao ndani ya chama au nje ya chama, wakati ambao kulikuwa hakuna chama kingine.

"Maalim aliona huko mbele lazima kuwe na mageuzi, yakatokea na vyama vikatokea, akatuachia wajibu huu ambao tunapaswa kuutekeleza. Na mimi ninawaahidi wananchi wa Pemba, Wazanzibar tutakuwa nanyi wakati wote.

"Tuwe ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa au nje ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, tupigwe mabomu au tusipigwe mabomu, tutekwe au tusitekwe, tuumizwe au tusiumizwe, tutakuwa nanyi mpaka pale tutakapohakikisha haki zinaheshimiwa na Zanzibar yenye mamlaka kamili inafikiwa," alisema.

Zitto alifafanua kuwa ameona aseme maneno hayo kwa kuwa wanao wajibu wa kukumbushana.

Alisema hawako kwenye siasa kwa sababu wanapenda kuwa huko, bali kwa sababu kuna masuala ambayo wanayapigania, ikiwa ni pamoja na haki za watu, uwajibikaji na demokrasia.

Alisema hiyo ndio sababu wanapigania mchakato wa Katiba Mpya ili waipate itakayojali haki za watu, uongozi unaowajibika kwa watu na itakayojenga mwafaka wa kitaifa.

Alisema wanaitaka serikali kwa haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa mapendekezo yaliyotolewa kwenye taarifa ya kikosi kazi, taratibu na mchakato wa Katiba Mpya uanze mara moja.

Pia alisema suala la sheria ya uchaguzi ili kuwa na Tume Huru ya Uchaguzi kupitia sheria mpya ya uchaguzi na sheria ya vyama vya siasa ni mambo ambayo yanapaswa kukamilishwa ndani ya mwaka huu kabla ya uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwakani na Uchaguzi Mkuu 2025.

"Sisi kama viongozi, hatutaki tena kushuhudia vizuka na yatima wakiwa mbele yetu kwa sababu tu kuna watu wachache wanataka mamlaka ya kisiasa," Zitto alisisitiza.

Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu alisema hawatokubali Uchaguzi Mkuu ujao ufanyike kwa kuwa na kura ya mapema. Pia alisema watapambana kuhakikisha Mkurugenzi wa sasa wa Uchaguzi Zanzibar anaondoka kwenye nafasi hiyo.

## MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA

# Karipio lake kwa mawaziri, makatibu linavyoangukia anakolenga kiuchumi

**Na Peter Orwa**



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

MWISHONI mwa wiki iliyopita, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan alifanya uamuzi mgumu wa kuja na mabadiliko katika safu yake ya serikali. Ni hali iliyogusa mabadiliko ngazi ya mawaziri, baraza lao, hali kadhalika watendaji wakuu serikalini.

Hapo kama ilivyo kawaida ya mitandao ya mawasiliano nayo ikaja na sauti nyingi, wapo waliomkosoa Rais, vilevile waliompongeza, kama kawaida umma nao ukimfuatilia.

Siku ya kuwaapisha, Rais Dk. Samia 'akawatolea uvivu' waliomkosoa akiwapa ufafanuzi wao na 'salamu juu', hali kadhalika akaorodhesha vigezo vya kiufundi kufikia alichoamua, akianika uhalisia wa serikalini.

Ni orodha iliyojumuisha alichokitaja 'kukerwa na ugomvi usioisha', hasa kada za mawaziri na naibu wao, pia makatibu wakuu na naibu wao, hata kati ya makundi ya vyeo hivyo, ikizingatiwa wote wako katika wizara moja na wanahusiana moja kwa moja kikazi.

Pili, Rais Dk. Samia akataja anahamishia jukumu la Uwekezaji, kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, akiiweka kwenye ofisi yake, akaanza na uteuzi wa Katibu Mkuu kuweka mambo sawa.

La tatu, akaelekeza lenye unasaba na misuguano, akishangaa muda mrefu tangu aagize kuidhinishwa madarakani Kamishna wa Tume ya Madini, lakini kukatawaliwa na kusuasua uamuzi bila ya sababu ya wazi. Siku hiyo, akaamua kumuidhinisha rasmi kamishna huyo.

Nne, akajibu ya mtandaoni akianika kwamba ameamua kuendelea kuwaingiza madarakani wasomi, ili umma ufaidike na uelewa wao, pia kada hiyo imekuwa ikichangia kulaumu serikali, sasa ni zamu yao kuona na kutenda magumu yaliyomo ndani ya utumishi umma.

Alhamisi wakiwa wamehamia jijini Arusha kwenye semina ya viongozi hao, siku mbili baada kuwaapisha, Rais Dk. Samia, msomi wa Utawala wa Umma, kutoka kilichokuwa Chuo Cha Uongozi wa Maendeleo Mzumbe (IDM), akataja kufanikiwa mipango yake mingi ya nchi ikiwamo siasa, akilalamika bado kuna shida kwenye safu ya uongozi.

### MAANA YAKE NINI?

Kimsingi, nguvukazi ambayo ametaja Rais Dk. Samia, ina mengi na maana kubwa katika uzalishaji. Uchumi nadharia yake inataja vyanzo vikuu vya uzalishaji ni: Nguvukazi ya mtu, mtaji, ardhi na nyenzo ya uzalishaji. Hata hivyo, ndani yake nguvukazi au rasilimali watu, inabaki katika nafasi kubwa ya kusimamia rasilimali zote zilizobaki muhimu kwa uzalishaji.

Katika nguvukazi, kati yao kuna viongozi wa ngazi mbalimbali kuanzia taasisi binafsi, hadi zile za kiserikali zilizopo katika ngazi ya juu wanakopatikana mawaziri na makatibu wakuu wa serikali, ambao Rais Dk. Samia anawanyooshea kidole cha kutoridhishwa na baadhi ya mambo kutoka kwao.

Alhamisi iliyopita 'watuhumiwa' hao walikusanywa jijini Arusha na kuaanza semina maalum ya kuwanoa kitaalamu katika stadi za uongozi na maadili, warejee katika nafasi zao kiuongozi na kusimamia vema uchumi wa taifa.

### KIONGOZI NI NANI?

Wanazuoni wa uongozi kama Rais Dk.Samia, wana tafsiri kwamba ni mtu anayepewa jukumu la kuwaonyesha njia walio chini yake. Mara nyingi kiongozi wa mfano, anatajwa ni yule anayejiamini, akiendana na matendo ya mfano.

Pia, penye dhana uongozi, ndani yake kuna stadi kuu mbili; Utawala na menejimenti: Wakati utawala unabaki kuwa namna ya kusimamia mwenendo wa kila siku biashara, taasisi ya chombo fulani; Menejimenti inazama katika kuratibu na kusimamia malengo yaliyowekwa mahali husika pa mtawala.

Hapo kunatajwa ndani yake kuna kuweka mipango, kufanya uamuzi bora, kuratibu malengo, kuongoza, kuhamasisha na kusimamia raslimali zote kama vile nguvu kazi, fedha, na mali nyinginezo.

Kwa maana hiyo, kiongozi wa umma kama vile Waziri na Katibu Mkuu, anapaswa kuwa na stadi hizo kusimamia raslimali zenye uhai na zisizo na uhai katika maeneo yake ya kazi. Hapo anakuwa tayari ameshanza kutoa mchango kwenye kujenga uchumi katika ngazi kubwa kisekta.

### VIONGOZI NA UCHUMI

Rais Dk. Samia akiwa ana wiki kadhaa kusherehekea miaka miwili ya uwapo wake katika uongozi, analia na kasoro katika menejimenti na utawala wa rasilimali ya taifa ambako kuna mipango na malengo yake, akiwa msimamzi mkuu anayesaidiwa kisekta na mawaziri na makatibu wakuu tajwa.

Ni maeneo ya kiuchumi yanayofunikwa na rasilimali za kina kitaifa, kuanzia watu na viumbehai vingi kitaifa, pia visivyo na uhai, mathalani madini, ardhi, bahari na maliasili.

Siku zote, nadharia uchumi, tafsiri yake inabaki kuwa namna sahihi ya kutumia rasilimali kidogo iliyoko kibusara, kukidhi matakwa na mahitaji makubwa ya kundi kubwa la wahitaji walioko. Hivyo, inarejewa kuwa mawaziri ambao ndio wasaidizi wakuu wa Rais Dk. Samia katika maeneo ya kisekta kwenye wizara, katika nafasi zao za uongozi wana wajibu wa kiuongozi kuonyesha dira bora, hata wakasimamia na kuratibu mwelekeo.

Ni mahali ambako tafsiri ya Rais Dk. Samia anapigana nayo ichukue nafasi, kwa wakuu wa wizara (mawaziri) na watendaji wakuu, makatibu wakuu.

Rais katika nafasi yake, ana dira kuu ya kitaifa inayopatikana kwenye mipango mikuu iliyoko, malengo kisekta, hali kadhalika uamuzi binafsi wa maendeleo anaobuni, pia miradi aliyorithi, mfano Mradi wa Umeme Stigler's Gorge na wa reli ya umeme, Standard Gauge.

Hiyo ikatoa wajibu kiapo kwa wateule wanaotumikia kuongoza wizarani ambao Rais Dk, Samia anawaanika 'wana tatizo', kujirekebisha kuwa timu moja kuhakikisha mfumo wa uchumi unasonga katika malengo yake.

Zao la kujirekebisha kiuongozi, huzaa ubunifu, bidii, mshikamano na kujitoa kazini, vyote vikielekeza majibu ya uzalishaji na mali na huduma bora kitaifa, ambayo tafsiri kuu inaangukia uchumi bora.

Kimuundo, uchumi huendana na uzalishaji wa huduma na mali za kibiashara, ambayo huzalisha fedha na mali, huku ununuzi na mauzo nazo zikikua.

Hatua yake inayopigwa ndio inafungua mzunguko wa fedha kupitia kukua shughuli za kibinadamu, kipato cha serikali kwenyea kodi, uwezo wa kupatia huduma za msingi kwa watu wake kama vile elimu, umeme, maji na matibabu.

Vilevile kunashuhudiwa kukua sekta kama za miundombinu, nishati, madini, ujenzi, teknolojia na ufundi, michezo, ustawi, makazi na matumizi ya ardhi inatanuka kwa kasi kubwa, huku nako matumizi bora ya fedha za umma na binafsi, inarejesha manufaa ya maendeleo kwa umma wa KItanzania.

Tafsiri ya ukali wa Rais Dk. Samia dhidi ya mawaziri na makatibu wake wakuu, inasimama katika nadharia ya uongozi ambako kuna mawaziri na makatibu wakuu aliyowakabidhi funguo kumsadia kutekeleza anayoyalenga kisekta, miradi, bajeti, mipango na malengo yake binafsi, katika tafsiri pana ni mafanikio kiuchumi.

Msingi wa taifa lolote hujengwa kwa mchango wa kila aliyemo kwa nafasi yake, kama usemi alioutoa Rais Julius Nyerere mwaka 1964 baada ya kuzindua Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano, ukiwa na mwongozo wa mipango na utawala; 'It Can be Done, Play your Part' ikimaanisha 'Inawezekana, Timiza Wajibu Wako.'




Viongozi wa serikali wakiwa katika semina jijini Arusha. **PICHA ZOTE : MPIGA PICHA WETU.**

## HABARI KITAIFA



Meneja Msaidizi Huduma za Ufundi kutoka Bodi ya Mfuko wa Barabara, Mhandisi Rashid Kalimbaga, akitia saini mkataba wa ushirikiano wa uanzishaji na uendeshaji wa mpango wa tathmini ya barabara Tanzania, Dar es Salaam juzi, wakati wa warsha ya kufunga mradi wa majaribio ya mpango wa hatua kumi 'Ten Step Plan' kuhusu miundombinu salama ya barabara nchini. Kushoto ni Mwenyekiti wa Chama cha Barabara Tanzania, Joseph Haule. **PICHA: THERESIA MWAMI.**

# RC akemea wagonjwa kupelekwa kutibiwa kwa waganga wa jadi

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko amewataka wananchi wa mkoa huo kuacha imani potofu za kwenda kutibiwa kwa waganga wa kienyeji pindi yanapotokea magonjwa ya mlipuko, akionya kuwa kitendo hicho huchangia vifo.

Mrindoko alitoa angalizo hizo juzi wa uzinduzi wa Mradi wa Shinda Malaria mkoani Katavi uliofanyika kwenye Kijiji cha Vikonge, Kata ya Tongwe, Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, ukitekelezwa kwa miaka mitano kuanzia Agosti mwaka jana.

Alisema kitendo hicho kimekuwa kikisababisha baadhi ya watu kucheleweshwa kufikishwa vituo vya afya ili kupatiwa matibabu sahihi.

Kiongozi huyo aliwataka wananchi kujenga tabia ya kuwahi kwenye vituo vya huduma za afya pale wanapougua ili kupata ushauri na kupatiwa matibabu sahihi. "Tunafahamu yapo maradhi mbalimbali, kuna malaria ambayo leo tunaizungumzia, katika mkoa wetu kuna baadhi ya maeneo yamekumbwa na ugonjwa wa surua, hasa kwa watoto, ninafahamu wameugua pia watu wazima.

"Baadhi ya watoto kwenye maeneo ya mkoa wetu wamepoteza maisha kwa sababu ya kucheleweshwa kufikishwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kutokana na wazazi wao kuanzia kwa waganga wa tiba asili kabla ya hospitalini," alisema.

Mrindoko aliwaeleza wananchi kwamba sio kila maradhi yanatibiwa kwa tiba asili.

"Tiba asili zipo na tunaziheshimu, lakini suala hili la surua na magonjwa mengine ya kuambukiza tiba zake ziko hospitalini, niwaombe sana wananchi wa Mkoa wa Katavi nendeni hospitalini kwa maradhi haya na mengine," aliagiza.

Kiongozi huyo aliwataka wananchi waliopimwa na kukutwa na malaria katika uzinduzi huo, kuzingatia matumizi ya dawa walizopatiwa na wataalamu.

Mkurugenzi Mkuu wa Mradi wa Shinda Malaria kutoka Taasisi ya Afya Ifakara, Dk. Dunstan Bishanga alisema mkoa huo ni kati ya mikoa saba ambayo wizara imeitambua kama mikoa yenye maambukizi ya juu ya ugonjwa wa malaria.

Alisema hiyo ndiyo sababu Shirika la Marekani la Maendeleo ya Kimataifa (USAID), kupitia Mfuko wa Kupambana na Malaria wa Rais wa Marekani (PMI) liliamua kuwekeza nguvu mkoani humo ili kupunguza maambukizi na vifo pamoja na madhara.

Mwakilishi wa USAID kupitia PMI, Lulu Msangi alisema PMI imeendelea kushirikiana na serikali kuhakikisha huduma za malaria zinapatikana kwa wananchi walio kwenye maeneo magumu kufikika.

Alisema juhudi zilizofanyika zimesaidia kupunguza kiwango cha maambukizi ya malaria nchini kutoka asilimia 18 mwaka 2015 mpaka asilimia nane mwaka 2020.

Mwakilishi wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Regina Joseph aliitaka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa huo na zinazohusika na masuala ya afya, kuhakikisha zinawafuatilia wadau hao na kujitathimini pale wanapofanya nao kazi ili kujua ni kwa kiwango gani watapunguza ugonjwa huo.

Katika uzinduzi huo, kati ya watu 100 waliofanyiwa vipimo vya ugonjwa wa malaria, 29 wakiwamo watoto 17, walikutwa na maambukizi, sawa na asilimia 29.

# Watoto wa miaka minane wanajisiwa

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

WANAFUNZI wawili wa kike wenye umri wa miaka minane, wanadaiwa kunajisiwa katika matukio tofauti katika wilaya za Mbogwe na Geita mkoani hapa, likiwamo lililotokea katika kijiji cha Luezela wilayani Geita.

Watuhumiwa wa matukio hayo wanashikiliwa na polisi na baada ya upelelezi kukamlilika, watafikishwa mahakamani

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Geita, Kamishna Msaidizi (ACP) Safia Jongo, alisema hayo juzi ofisini kwake wakati akitoa wito kwa jamii na wazazi kuchukua tahadhari kukabiliana na wimbi la vitendo vya ubakaji kwa watoto.

Jongo alisema katika tukio lililotokea Februari 24 katika kijiji cha Luezela, Majiko Said mwenye umri wa miaka 62, alimnajisi mwanafunzi mwenye umri wa miaka minane wakati akienda shuleni baada ya kumnunulia muwa na kisha kumkamata.

Alisema baada ya kumnunulia muwa mwanafunzi huyo, mtuhumiwa alimfuata kwa nyuma mtoto huyo na walipoingia katika eneo la shule anayosoma mtoto huyo, alimkamata na kuziba mdomo na kumbana mikono na kisha kumvutia katika kichaka na kuanza kumtendea ukatili huo.

Wakati akiendelea na kitendo hicho, alisema msamaria mwema aliyetambuliwa kwa jina la Fitina Misungwi, alitokea na kisha kuita mtu mwingine waliosadiana kumwokoa mwanafunzi huyo na kumkamata mtuhumiwa ambaye alikabidhiwa kwa uongozi wa kijiji.

Tukio lingine, Kamanda Jongo alisema lilitokea wilayani Mbogwe wiki iliyopita kwa mwanafunzi wa darasa la kwanza kunajisiwa na mtu mzima wakati akitoka shuleni kurudi nyumbani. Alisema mtuhumiwa alimkamata mtoto huyo na kumvutia kichakani ambako alimtendea ukatili huo.

Akizungumzia ukatili uliotokea wilayani Geita, Misungwi aliyeongoza kuokolewa kwa mototo huyo, alisema walimkuta mtoto huyo akiwa ameanza kuishiwa nguvu kutokana na kukosa pumzi baada ya mtuhumiwa kumziba mdomo na kumkamata mikono yake yote ili asipige kelele.

Misungwi alisema ukatili huo hauvumiliki na unahitaji kukemewa kwa nguvu zote na jamii bila kufumbiwa macho kwa kuwa bila msaada huo wa haraka, mtoto huyo angepoteza maisha.

Awali, Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Samson Walwa, alisema baada ya kupata taarifa walimkamata mtuhumiwa na kumkabidhi polisi kwa hatua zaidi za kisheria.

Mmoja wa watoto aliyefanyiwa kitendo hicho, alisema ilikuwa majira ya saa 4:30 asubuhi na mtuhumiwa alimshawishi kumnunulia muwa na baada ya hapo alimfuata kwa nyuma kisha kumkamata na kumvutia vichakani na kumziba mdomo na kumvua nguo za ndani na ndipo alipoanza kumtendea ukatili huo.

Baadhi ya wazazi na wanajamii walioguswa na madhila hayo wamejitokeza na kupaza sauti kwanza, kuwashukuru wasamaria wema waliomwokoa mtoto wao kwa kuwa bila kupata msaada wa haraka, angepoteza maisha.

# Rais adhamiria walengwa TASAF kuwa na maisha bora

**Na James Mwanamyoto,** SIHA

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Jenista Mhagama, amesema Rais Samia Suluhu Hassan amedhamiria kila mlengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), anaishi maisha bora.

Mhagama alisema hayo jana alipokuwa katika vijiji vya Wiri na Ngumbaru, wilayani hapa akikagua utekelezaji wa mpango huo.

Alisema Rais Dk. Samia alipoingia madarakani aliamua kuendelea kutekeleza mpango huo ili kuboresha maisha ya wananchi walio katika kaya maskini.

"Nimeenda kujionea mwenyewe namna walengwa wa TASAF walivyoanzisha miradi ya kufuga kuku, mbuzi na ng'ombe na wengine wamejenga nyumba za kuishi," alisema Mhagama.

Waziri pia alisema uamuzi huo umewawezesha watoto wa walengwa wa TASAF kupata elimu bora na huduma bora za matibabu kupitia utekelezaji wa miradi ya elimu na afya na kuongeza kuwa katika maeneo mengine walengwa wamejiunga na bima ya afya inayowasaidia kupata huduma ya matibabu kwa urahisi.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete, alisema amejionea mafanikio ya walengwa wa TASAF wilayani Siha na kuongeza kuwa pamoja na mafaniko hayo bado Rais anaendelea na jitihada zake za kutafuta fedha ili zitumike kuboresha maisha ya Watanzania wengi zaidi.

Kikwete aliwataka Watanzania kuendelea kuwa na imani na Rais Samia ambaye ameonyesha nia ya dhati ya kuboresha maisha ya wananchi anaowaongoza, hivyo walengwa wa TASAF hawana budi kumuunga mkono kwa kutumia vizuri ruzuku wanayoipata kuboresha maisha yao.

Mmoja wa walengwa hao katika kijiji cha Ngumbaru, Kilei Kessy, alimshukuru Rais Samia kwa kuboresha maisha yao kupitia ruzuku ya TASAF.

Kessy alisema walengwa wa TASAF katika kijiji chao wanaendelea vizuri kwa kuwa kupitia mfuko huo wamepata uwezo wa kuwapeleka watoto wao shuleni, kujishughulisha na ufugaji na kujenga nyumba bora ambazo wanaishi na familia zao.

Mpango wa kunusuru kaya maskini nchini umeziwezesha kaya maskini kupata huduma bora za afya, elimu na kuboresha maisha yao kwa kuongeza kipato kupitia ufugaji, kilimo na ujasiriamali.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kwa hili la MSD kunahitajika kuwapo ufumbuzi wa kudumu

**KWA** muda mrefu kumekuwa na taarifa za kukosekana kwa dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya, kwa maana ya hospitali, vituo vya afya na zahanati, katika maeneo mbalimbali nchini.

Hivi karibuni, katika wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, kwa mfano, ilibainika kuwa vituo vingi vya afya na zahanati havina dawa na vifaa tiba kutokana na kucheweshwa kupelekwa na licha ya kuilipa Bohari Kuu ya Dawa (MSD). Tatizo hilo pia liliibuka juzi wakati wa ziara ya sekretarieti ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ikiongozwa na Katibu Mkuu, Daniel Chongolo mkoani Singida.

Chongolo na timu yake katika ziara hiyo, walifika katika hospitali ya wilaya ya Singida na kubaini kuwa miundombinu yote imekamilika lakini tatizo lililopo ni ukosefu wa vitanda na vifaa vya maabara. Viongozi hao wa CCM walielezwa kuwa vifaa hivyo vinakosekana licha ya kwamba vimeagizwa kutoka MSD.

Kutokana na hali hiyo, Katibu Mkuu huyo aliiagiza Wizara ya Afya kuweka bayana mpango wa bohari hiyo wa kusambaza dawa na vifaa tiba katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini ili wananchi wapate huduma. Hakuishia hapo tu bali alisema atakaa na wizara ili kujua suala hilo litapatiwa ufumbuzi lini kwa kuwa kumekuwa na kilio kama hicho kila kona ya nchi.

Kwa ujumla suala la MSD kulipwa fedha na kushindwa kupeleka dawa limekuwa likilalamikiwa katika maeneo mbalimbali hatua ambayo ilisababisha hata viongozi wa juu serikalini akiwamo Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, ambaye alitoa maagizo ya kumaliza tatizo hilo alipokuwa katika ziara mkoani Mwanza.

Uwapo wa tatizo hilo na hata kukemewa na viongozi wakuu, limekuwa sasa ni kama sikio la kufa lisilosikia dawa. Ni dhahiri kwamba katika hilo, kuna jambo la kufanywa ili kumaliza malalamiko hayo ambayo ni kama hadithi isiyokuwa na mwisho.

Jambo la kujiuliza ni kwa nini MSD ipokee fedha kutoka kwa wateja, ambao ni vituo vya kutolea huduma za afya na kushindwa kutoa huduma stahili? Tatizo hasa ni nini? Je, mfumo wa uagizaji dawa, uhifadhi na usambazaji vina kasoro au changamoto gani? Inakuwaje taasisi inapokea fedha na kushindwa kutoa huduma kwa wakati na matokeo yake kusababisha wananchi kukosa huduma wanazohitaji?


Maswali hayo hayana budi kupatiwa majibu ili kubaini chanzo cha tatizo. Yako mambo kadhaa ambayo yamefanyika ndani ya taasisi hiyo nyeti yakiwamo mabadiliko ya viongozi wanaoiongoza lakini inaonekana dhahiri kwamba hayajasaidia chochote. Kwa maneno mengine, huenda mabadiliko hayo yalikuwa sawa na kutibu kidonda bila kutambua chanzo chake, hivyo uchunguzi wa kina ufanyike ili kubaini tatizo na hatimaye kupatikana kwa ufumbuzi wa kudumu.

Ni dhahiri kwamba uchunguzi wa kina utakapokamilika, kuna majibu yatakayopatikana kuhusu matatizo yaliyopo na hatimaye kuchukua hatua ikiwamo kufumuliwa kwa taasisi na kusukwa upya ili kupatikana kwa tija na ufanisi.

Inavyoonekana ni kwamba kuna mfumo wa ukiritimba uliowekwa kwamba vituo vyote vya serikali vya kutolea huduma za afya vinatakiwa kuchukua dawa MSD na kwa kulipa fedha kwanza kabla ya kupata huduma husika. Ni vyema pia suala hilo likaangaliwa ili kupata ufumbuzi na mfumo sahihi wa kuwezesha kupatikana kwa dawa na vifaa tiba kwenye vituo hivyo.

Kubwa zaidi linaloweza kufanywa ni kushirikisha watoa huduma binafsi kwa maana ya sekta binafsi kushirikishwa katika uuzaji na usambazaji wa dawa na vifaa tiba kwa bei elekezi. Ni wazi kwamba suala hilo linaweza kupunguza kwa kiasi fulani malalamiko ambayo yametamalaki hivi sasa katika maeneo mbalimbali.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Vigogo wizarani kugombana ni ukosefu wa nidhamu

Na Sabato Kasika

**KWA** kawaida huwa ni heshima kubwa pale watu wanapoteuliwa na Rais kushika nafasi fulani ili kumsaidia kuongoza serikali, katika ngazi mbalimbali kuanzia wizara, mikoa, wilaya na kwingineko.

Uteuzi huo huonyesha imani ya Rais kwao na pia kiongozi huyo wa nchi huwa na mategemeo makubwa ambayo huwa ameweka kwa wateule hao ili kumsaidia majukumu ya kuongoza nchi katika ngazi alizowaweka.

Hata hivyo, kinyume cha matarajio yake, baadhi ya wateule ambao badala ya kutimiza majukumu ambayo Rais amewapa, wanabadilika na kufanya aibu kwa kugombana na kuisababishia serikali fedheha. Wako baadhi ya wateule au wasidizi wa Rais katika ngazi mbalimbali ambao wamegeuka kuwa sehemu ya tatizo badala ya kuwa sehemu ya suluhisho la matatizo ya maeneo wanayoongoza.

Miongoni mwa mambo ambayo wanatuhumiwa kuendekeza, ni ugomvi binafsi, kitendo ambacho ninadhani kinaweza kukwamisha maendeleo, hasa kutokana na ukweli kwamba ugomvi unasababisha wasishirikiane.

Wamekuwa wakiendekeza ugomvi binafsi mpaka kufikia hatua ya kutoleana lugha zisizofaa, kuwekana ndani, Ugomvi huo kwa ujumla ni kwamba, unarudisha nyuma jitihada za Rais za kuleta maendeleo ya nchi, kwani hawawezi kukaa pamoja kuweka mikakati na mipango ya maendeleo kwenye maeneo yao ya nchi kwa ujumla.

Kimsingi, sijaelewa kiburi cha wateule kugombana wanakitoa wapi. Ninachoamini ni kwamba sifa ya msingi ambayo viongozi wote wanatakiwa kuwa nayo ni busara na hekima.

Sifa hizo zinaweza kuwaongoza kujua kipi wakizungumze, wapi wazungumze, ingawa katika vikao vya ndani vya kazi inaweza kutokea watu kutoelewana au kupishana lugha, lakini mambo ya ndani ya vikao huishia katika vikao.

Haipendezi mambo ya ndani ya vikao kuyapeleka nje ya vikao au kiongozi kukosolewa na kuamua kuwa na 'bifu' dhidi ya mwenzake, tabia hiyo ninadhani haifai kwa kiongozi iwapo hataki kukosolewa.

Ni kutokana na ugomvi huo, Rais Samia Suluhu Hassan anaamua kuwapangua kutoka wizara moja kwenda nyingine, huku akionyesha kukerwa na tabia hiyo na kuahidi kuwatupa nje watakaobainika kuendekeza.

Anakaririwa na vyombo vya habai akisema: "Ni jambo ambalo silipendi mtu kutokuelewana, mawaziri na manaibu na makatibu wake. Sasa ni mwisho kupangua mmoja mmoja kwenye wizara. Ikitokea tena, mtaondoka wote kwa pamoja"

"Hili silipendi, ninataka nikiwapanga mfanye kazi, sioni sababu ya kutokuelewana, sizielewi sababu zenu za kutokuelewana," ndivyo anavyosema Rais Samia katika lugha ya ukali.

Ninadhani kauli hiyo ya Rais inatosha kuwafanya watimize wajibu wao, wakumbuke viapo walivyokula, maelekezo ya ilani ya chama, fikra na maono ya Rais katika kuupiga vita umaskini, sio kugombana wenyewe kwa wenyewe.

Vilevile, ni jambo la kawaida kwa viongozi kuwa na kauli moja hadharani, lakini kauli zinazotofautiana wateule wa Rais katika suala moja, zinaibua maswali katika dhana ya uwajibikaji wa pamoja.

Ikumbukwe kuwa katika dhana hiyo, viongozi hutakiwa kuwa na kauli moja kuhusu jambo fulani, hata kama katika vikao vya ndani huwa wanatofautiana, kwani hilo linafanyika kwa lengo la kutoyumbisha wananchi.

Kwa mazingira hayo ya kuachana hivyo, inawezekana ndicho chanzo cha baadhi ya wateule kugombana, kitendo ambacho ninakichukulia kama ukosefu wa nidhamu kazini na aibu kwao.

Wale ambao ni wahenga na wafuatiliaji wa muziki wa dansi, watakuwa wamewahi kusikia baadhi ya maneno ya wimbo ulioimbwa na bendi moja ukielezea umuhimu wa nidhamu kazini inavyoepusha migogoro.

Maneno yenyewe ni haya; "Nidhamu ya kazi, ni msingi, wa mafanikio mema kazini, viongozii na wafanyakazi lazima wote tuwe na nidhamuuuu. Migogoroooo na migongano ya kazini ni ukosefu wa nidhamu."

FIKRA MBADALA

# Wanawake wana uwezo kuliko wanaume, wawezeshwe zaidi



Pascal Mayalla

TUNAPOELEKEA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8, kila mwaka, leo naomba tujadili uwezo wa wanawake kwenye baadhi ya maeneo.

Kuna wanawake wana uwezo mkubwa kuliko wanaume lakini wamekuwa wanafunikwa na mfumo dume. Wakipewa fursa za kuonyesha uwezo, watafanya makubwa kuliko hata wanaume.

Mifano iko mingi, kuna wanawake wakati wakiwa na waume zao, waliishi maisha ya kawaida lakini baada ya kufiwa na kubaki wajane, wakafungua nguvu za uwezo na sasa wanaishi maisha mazuri kuliko hata waume zao walipokuwapo.

Japo kazi ni kazi tu, hakuna kazi za kike wala za kiume. Kuna ukweli kuwa kwenye baadhi ya kazi, wanawake wana uwezo kuliko wanaume, ikiwamo ile kazi ya uumbaji wa kiumbe kipya, japo hufanywa kwa ushirikiano wa jinsia mbili, lakini uumbikaji wa kiumbe kipya kinaumbikia ndani ya jinsia ya kike pekee, hivyo ni mwanamke pekee ndiye huweza kuumba na kuleta kiumbe duniani, hivyo mwanamke ana uwezo kuliko mwanamume.

Baada ya kiumbe kipya kuzaliwa, kazi ya ulezi wa mwanzo, ya kunyonyesha, hufanywa na wanawake tu na kufanya wanawake kuwa ndio walezi bora wa familia, hivyo kazi zote za kulea watoto wadogo hufanywa na wanawake.

Tena wanawake hawaishii kwenye ulezi wa watoto wadogo tu bali ni pamoja na familia kwa maana hiyo, hulea hata yule 'mtoto mkubwa' wa familia ambaye anatambulika kama kichwa cha nyumba au nguzo ya familia kwa pale sebuleni tu, kibarazani, kiambazani na mitaani, lakini chumbani, mtoto mkubwa naye pia analelewa tu kama mtoto.

Kwa mantiki hiyo, hakuna ubishi kuhusu uwezo wa wanawake kwenye baadhi ya maeneo. Wanawake wana uwezo mkubwa kuliko wanaume kwenye mambo mengi tu, hata katika uongozi.

Tena ni ukweli usiofichika kuna baadhi ya kazi zinazohitaji miguvu, zinawafaa zaidi wanaume kuliko wanawake. Kuna baadhi ya wanawake wana maumbile ya kike lakini wana nguvu kuliko wanaume na wanaweza kufanya kazi zote za kiume na wakati huo huo, kuna wanaume wana maumbile ya kiume lakini ni walaini kupita hata wanawake kwa hiyo hawawezi kufanya kazi za kiume.

Si wengi wanaojua kuwa baada ya Mungu kuwaumba Adamu na Eva, au Adam na Hawa, mtu wa kwanza kabisa kufanya kazi ni mwanamke, ile kazi ya kuchuma tunda, ilifanywa na Eva au Hawa, akampelekea tunda Adamu na kumfundisha jinsi ya kula lile tunda ndipo Adamu akala na hii ndiyo kazi ya kwanza kabisa duniani, ikiitwa 'the oldest profession'.

Mwanamke ndiye pekee anaweza kufanya kazi zote lakini kuna kazi fulani fulani wanawake wanazifanya vizuri kuliko wanaume zikiwemo kazi za ndani, uhudumu, mapokezi, maonyesho ya mitindo, kucheza muziki na uhudumu wa vinywaji katika baa na hoteli.

Kuna kazi mfumo dume umezipachika kuwa ni kazi za kike, zikiwamo upishi, ubunifu wa mavazi, ususi na kazi za kuremba wanawake lakini imetokea wapishi katika hoteli kubwa (Chefs) wanaume! Wabunifu wakubwa wa mavazi ni wanaume, hata warembeshaji wakubwa na sasa wasusi ni wanaume.

Nenda saluni za kike ushuhudie idadi ya wasusi wa Kikongo au pita pale Mwenge Jumamosi asubuhi ushuhudie jinsi morani wa Kimasai wanavyokula tenda za kuwasuka rasta dada zetu.

Huu mfumo dume umesababisha baadhi ya nafasi kupewa majina ya kiume mfano Boss ni jina la kiume, boss akiwa ni Mwanamke anaitwa 'The Boss Lady', lakini mabosi wa kike wanapenda kuitwa Boss na wafanyakazi wengi wanapendelea boss awe mwanamume na si Mwanamke, maana boss akiwa ni mwanamke, kuna fikra kuwa kuna watu wanakoma.

Pia nafasi kama ya 'Chairman' au Mwenyekiti ni jina la kiume, akiwa mwanamke alipaswa kuitwa Chairwoman ila ikaonekana hainogi, hivyo Mwenyekiti akiwa mwanamke anaitwa 'Chairperson'.

Hata cheo cha 'President' na Amiri Jeshi Mkuu kilidhamiriwa kuwa ni cheo cha mwanaume, mwanamke anaitwa Amirati, ila hata Amiri Jeshi Mkuu anapokuwa mwanamke, hapendi kuitwa Amirati anapenda kuendelea kuitwa hivyo hivyo Amiri Jeshi Mkuu ambalo ni jina la kiume.

Makala hii inahusu fupa fulani ambalo ukimwondoa Baba wa Taifa aliyetuachia Katiba ya Tanzania ya mwaka 1977, marais wanaume wanne walioufuatia, hilo fupa liliwashinda maraisi Ali Hassan Mwinyi, Benjamin Mkapa, Jakaya Kikwete na John Magufuli liliwashinda lakini sasa tuna rais mwanamke, Samia Suluhu Hassan ambaye ameshaonyesha kila dalili atelishinda. Fupa hilo ni la katiba. Wanaume walishindwa lakini mwanamke anaonyesha ataliweza.

Kwa hiyo wanawake wana uwezo kuliko wanaume kama watapewa nafasi. Naomba kuchukua fursa hii kuwatakia wanawake wote maandalizi mema ya Siku ya Wanawake Duniani, Machi 8.

**Paskali 0754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Mawaziri wetu hebu pambaneni na haya



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

ZAMANI shuleni tulifundishwa nyimbo za uzalendo, mapambano dhidi ya dhuluma na za kutukuza taifa na viongozi wake lakini pia zikiwamo za kuhimiza kazi na afya.

Tuliimba nyimbo hizo madarasani katika matukio maalumu kama siku kuu, lakini pia kwenye mchakamchaka. Nyimbo hizo mbali na kutujengea ukakamavu, zilielimisha jamii kuhusu masuala mbalimbali.

Hivyo kila serikali ilipotoa tamko lililotakiwa kufika kwa jamii, wanafunzi tulitumika kuhanikiza ujumbe kupitia nyimbo hizo na hakika ulifika kwa waliokusudiwa.

Sambamba na kufundishwa nyimbo, pia miongoni mwa vipindi tulivyofundishwa vilikuwa vya dini na mara zote dini za Kikristo na Kiislamu. Hivyo wakati wa kipindi hicho, wanafunzi tuligawanyika madarasa.

Tulifundishwa dini si kwa ajili ya mitihani, la hasha, ilikuwa kwa ajili ya maadili, kumkumbuka, kumshukuru na kumwabudu Mungu. Yote hayo yalisaidia kuleta na kudumisha amani katika jamii.

Wakati huo shule za kimataifa zilizofundisha kwa mtaala wa Kiingereza hususan za binafsi hazikuwapo maeneo mengi, hivyo kubakiwa na shule za serikali.

Kutokana na hali hiyo, mitaala ilifanana, hakukuwa na utofauti wa mafunzo kati ya shule moja na nyingine, hivyo kama mwanafunzi alihama shule moja kwenda nyingine hakubaini tofauti kubwa.

Taratibu mambo haya yakaanza kufutika, nyimbo zikafundishwa zisizo za kizalendo hata katika shule zetu za serikali, watu wakasahau hata kuimba Wimbo wa Taifa!

Fuatilia leo hata katika viwanja vya michezo, mathalan timu ya soka ya taifa inapokuwa inacheza na nyingine ya kigeni, upigwapo au uimbwapo Wimbo wa Taifa, angalia ni wachezaji wangapi wanaoimba.

Hiyo inaonyesha ni jinsi gani ama hawakutilia maanani kujifunza au hawakufundishwa kabisa shuleni walikosoma. Mmomonyoko wa uzalendo unaanzia hapo.

Hivi karibuni, serikali ilibaini madudu katika baadhi ya shule nchini kwamba kuna vitabu vinatumiwa kufundisha tabia chafu miongoni mwa wanafunzi, vitabu vinafundisha mapenzi ya jinsia moja kwa wanafunzi.

Imechukua hatua ya kuvipiga marufuku vitabu hivyo na kuviteketeza kuanzia shuleni hadi kwenye maduka vinakouzwa ili kuokoa maisha ya kimaadili ya watoto.

Wazazi wametakiwa kuchukua hatua ya kukagua madaftari na vitabu vya watoto wao warudipo majumbani kutoka shuleni ili kusaidia kupambana na kadhia hiyo.

Unajiuliuza ni nini lilikuwa lengo la wenye shule kukaribisha vitabu hivyo shuleni mwao. Unabaini kuwa ni utandawazi ambao umewakumba Watanzania kama ilivyo kwa mataifa mengine.

Hivi sasa kuna wimbi kubwa la kutetea ndoa za jinsia moja, ushoga umekithiri kuanzia Ulaya mpaka Afrika. Kuna malumbano yanaendelea kati ya mataifa.

Kuna majibizano baina ya viongozi wa Kiafrika na wa Ughaibuni kuhusu ndoa hizo na mapenzi ya jinsia moja kwa ujumla wake. Yapo mataifa ya kiafrika yametoa msimamo wa kuzikataa.

Yako mataifa yamekaa kimya kana kwamba hayaoni kinachoendelea, kisa ni kuchelea kukosa misaada kutoka mataifa makubwa yanayotetea na hizo za kifirauni.

Tanzania si kisiwa, hivi sasa wanafunzi shuleni wameachana na nyimbo za kizalendo, wanaimba nyimbo za mapenzi zinazoimbwa na wasanii wetu wa kizazi kipya.

Hivi sasa si mara moja kusikia hata kwenye mabasi ya shule wanafunzi wakiimba nyimbo kama 'Bia Tamu', 'Amelowa' na kadhalika, tena kwa furaha na bashasha. Maana yake wanafundishwa shuleni.

Wanafunzi kidogokidogo wanatoka kwenye mstari na kufanya yuasiyoendana na wanachofundishwa shuleni, wanafanya wanayojua wao, wakidhani ndiyo yanakidhi matamanio yao.

Tanzania kuna wanamuziki na wasanii, wanamuziki wanaimba nyimbo zenye maadili, lakini wasanii wanaimba nyimbo zinazokengeuka maadili ya kibinadamu, kama hizo za kutukuza pombe na ngono.

Hatua madhubuti zisipochukuliwa, Taifa litaangamia kwa kuwa na watu wasio na maadili wala welewa wa mambo chanya kwa Taifa lao.

Waziri Nape Nnauye- angalia vyombo vyako vya habari, sikiliza watangazaji wanavyobananga lugha angalia pia nyimbo zinazoimbwa redioni na kwenye televisheni.

Naibu Waziri Hamisi Mwinjuma 'Mwana FA'- Rais Samia Suluhu Hassan amekuamini katika kusimamia wasanii na wanamuziki, wasimamie wasanii waache kabisa kutuimbia nyimbo za kifirauni. Watunge nyimbo zenye maadili na uzalendo.

Profesa Adolf Mkenda- shule zako zinakengeuka, zifuatilie kwa karibu, ili zisipotoshe watoto ambao bongo zao ni rahisi sana kukamata mambo yasiyo na maana na kuyatumia, mwishowe hatutakuwa na taifa bora. **Alamsiki!**

# CCM yacharuka mbolea ya ruzuku kuuzwa bei juu

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo ametoa maelekezo kwa Wizara ya Kilimo kuongeza vituo vya kuuzia mbolea ya ruzuku kutokana na baadhi ya maeneo kulalamikia kuuziwa kwa gharama ya juu na kutembea umbali mrefu kuifuata.

Chongolo alitoa maagizo hayo jana alipozungumza na wananchi katika shina namba mbili kata ya Mtinko wilayani Singida baada ya kupokea malalamiko kwa wananchi kwamba mbolea hiyo inapatikana kwa gharama ya juu licha ya kuwapo ruzuku iliyotolewa na serikali kutokana na umbali na vituo vichache.

Alisema uamuzi wa serikali wa kuweka ruzuku kwenye pembejeo, ikiwano mbolea, umebeba dhamira kubwa ya kupunguza mzigo wa gharama za uzalishaji.

"Wote mnajua mbolea ilipanda bei kwani serikali ndio ilipandisha bei? Hapana! Duniani huko wanakozalisha walikuwa wamejifungia kwa sababu ya ugonjwa wa corona, hivyo mbolea na mafuta yalipanda bei ikawa inauzwa kwa Sh. 140,000 hadi 160,000 (kwa mfuko)," alisema.

Chongolo alisema changamoto iliyojitokeza mwaka huu katika suala la mbolea itatafutiwa ufumbuzi, akifafanua kuwa mwaka uliopita wa kilimo ulikuwa mwaka wa majaribio lakini mwaka ujao kutakuwa na uhakika mbolea kuwafikia wananchi maeneo yote.

Alisema viwanda vinavyozalisha mbolea nchini kikiwamo cha Dodoma ambacho wakulima wameipenda mbolea yake, viongeze uzalishaji, akisisitiza haiwezekani kuendelea kuagiza na kutumia mbolea inayotoka nje ambayo kimsingi haiendani na mazingira ya nchini.

Mkuu wa Mkoa Singida, Peter Serukamba alisema kwa mara ya kwanza katika historia ya Tanzania bei ya mbolea imeuzwa nusu bei ambapo mwaka jana ilikuwa ikiuzwa kati ya Sh. 140,000 hadi 150,000 lakini mwaka huu serikali imetoa ruzuku zaidi ya Sh. bilioni 150 na hivyo kufanya kila mfuko wa kilo 50 kuuzwa kwa Sh. 70,000.

Serukamba alisema huko nyuma serikali ilishawahi kuweka ruzuku lakini ikatumiwa vibaya, hivyo mwaka huu serikali iliweka utaratibu ambao kila mwananchi anayehitaji mbolea alijindikisha kwenye vituo ili kulinda upotevu na kutokuondoa nia njema ya kusaidia wananchi kupata mbolea kwa bei nafuu.

Awali wananchi walilalamikia mbolea kuuzwa kwa bei ghali hadi Sh. 100,000 kwa mfuko wenye ujazo wa kilo 50 wakati wanafahamu serikali iliweka fedha za ruzuku kwenye pembejeo ikiwamo mbolea.

Wananchi hao walisema changamoto nyingine iliyojitokeza mwaka huu ni vituo vya kuuzia mbolea ya ruzuku kuwa mbali na wakulima, jambo ambalo limeleta usumbufu.

## MEWATA: Wanawake wengi hawana uelewa saratani

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA) kimefanya kongamano kubwa la kisayansi kujadili changamano za masuala ya afya hususani saratani ya kizazi na magonjwa yasiyo ya kuambukiza.

Vilevile, kimebaini wanawake wengi wana matatizo ya kiafya, ikiwamo saratani lakini wana uelewa mdogo wa maradhi hayo.

Kongamano hilo ambalo limekutanisha madaktari, wanasayansi na wadau mbalimbali wa masuala ya afya lilifanyika juzi Dar es Salaam na kufunguliwa na Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassoro Ahmed Mazrui.

Rais wa MEWATA, Dk. Zaitun Bokhary alisema wamejikita katika kupambana na magonjwa ya saratani yanayoshambulia wanawake kwa asilimia kubwa, ya mlango wa kizazi na matiti.

Pia alisema chama kinahamasisha watoto wa kike kujiunga na fani za udaktari ili baadaye wawe madaktari kwani huko nyuma fani hiyo ilikuwa ni kwa ajili ya wanaume tu.

Alisema hamasa hiyo imeleta mafanikio makubwa kwa kuwa sasa kuna idadi ya kutosha ya madaktari wanawake na inaendelea kukua.

Dk. Zaitun alisema chama hicho kimefanya mazoezi ya kupima afya za kinamama katika mikoa mbalimbali ikiwamo Dar es Salaam, Mbeya, Lindi, Mtwara, Kilimanjaro, Njombe, Iringa, Tabora, Dodoma, Songea na Mwanza.

"Katika mazoezi haya, tulifanikiwa kuwafanyia uchunguzi wa awali wa saratani ya matiti kinamama takriban 73,744 na uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi kinamama 9,307," alibainisha.

Alisema wamegundua wanawake wengi wana matatizo mengi ya kiafya hususan magonjwa ya saratani na uelewa mdogo wa maradhi hayo. "Hii imechangia wanawake wengi kuripoti hospitalini wakiwa wamechelewa au wako katika hatua za mwisho za ugonjwa na kuchangia vifo vingi vitokanavyo na saratani kwa kinamama," alisema.

Pia alisema pamoja na hilo, MEWATA kwa kushirikiana na serikali wamefanikiwa kuhamasisha wanafunzi wa kike wa sekondari kuchukua masomo ya sayansi na kuongeza idadi ya madaktari wanawake Tanzania na kuwajengea uwezo na kusababisha kuteuliwa kushika nyadhifa mbalimbali serikalini na taasisi binafsi.

Alisema MEWATA ina mpango wa kujenga hospitali kwenye eneo la Mbweni, Dar es Salaam kwa msaada wa Serikali ya Japan kupitia mama mlezi wa chama, Mama Salma Kikwete.

"Kwa sasa tumehamasishana wanachama na tumeweza kukusanya fedha taslimu Sh. milioni 31.5 na ahadi zikiwa ni Sh. milioni 46.5," alisema.

Kongamano hilo lilitarajiwa kufuatiwa na Mkutano Mkuu wa 20 wa MEWATA jana ikiwa ni maadhimisho ya miaka 35 tangu kuanzishwa kwa chama, ambacho malengo yake ni kusaidia, kuhamasisha na kutoa elimu kuhusu magonjwa na afya ya mama na mtoto.




Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui (kushoto), akikata utepe kuzindua kitabu kuhusu wasifu wa Mwasisi wa Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), Prof. Esther Mwaikambo (kulia), kwenye kongamano la 20 la kisayansi la chama hicho, Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watiwa mbaroni wakidaiwa kukutwa na meno ya tembo

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

JESHI la Uhifadhi Wanyamapori na Misitu, Hifadhi za Taifa (TANAPA) Ruaha, limewakamata watuhumiwa watatu wakiwa na meno manane ambayo hayajakatwa na vipande sita vya meno ya ndovu.

Idadi hiyo ya meno ni sawa na tembo sita wenye umri tofauti waliouawa wenye thamani ya dola za kimerakani 90,000 (Sh. milioni 206.8), kwa mujibu wa jeshi hilo.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha (RUNAPA), Kamishna Msaidizi wa Uhifadhi Godwell Ole Meing'ataki alibainisha hayo juzi wakati wa mkutano wake na waandishi wa habari mkoani Iringa uliolihusisha pia Jeshi la Polisi.

Alisema kuwa tukio hilo lilitokea Februari 20 mwaka huu majira ya 3:30 usiku kwenye Mtaa wa Mbombamili, Mawelewele, Kata ya Mivinjeni, Manispaa ya Iringa, akikiri kuwapo vitendo vya ujangili wa tembo na wanyama wengine kwenye hifadhi hiyo.

Ole Meing'ataki aliwashukuru wasamaria wema wanaoendelea kutoa taarifa kwa vyombo vya ulinzi huku akiwaliwaja watuhimiwa wanaodaiwa kukamatwa na meno hayo kuwa ni Greyson Lusasi (39), mkazi wa Mwangata 'D'; Elia Halamga (55), mkulima na mkazi wa Kateshi mkoani Manyara pamoja na Henry Chengula (38), mkazi wa Isakalilo mjini Iringa.

"Watuhumiwa hawa walikutwa na vielelezo mbalimbali kama vile kisu kimoja (jambia), msumeno mmoja na mifuko mitatu aina ya sulphate ikiwa na meno ya tembo yakiwa kwenye gari aina ya Noah lenye namba za usajili T 385 BWQ," alifafanua.

Hifadhi ya Taifa Ruaha ina idadi kubwa ya tembo wanaokadiriwa kufikia 15,000 kulingana sensa za hivi karibuni.

Meing'ataki pia alielezea kuwa tembo ndio kivutio kikubwa na alama ya uhifadhi kwenye hifadhi hiyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi wa Polisi Allan Bukumbi alithibitisha kushikiliwa kwa watuhumiwa kukamatwa waliokamatwa na nyara za serikali.

Alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na askari wa TANAPA, kwenye msako walifanyikiwa kuwakamata watuhumiwa hao wakiwa na nyara hizo za serikali.

Kamanda Bukumbi alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakiwa katika harakati za kutaka kufanya biashara na watu waliokuwa wakiwasiliana nao na watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Pia alisema Jeshi la Polisi Mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na maofisa wa Manispaa ya Iringa na maofisa wa LATRA, wamefanikiwa kukamata bajaji zaidi ya 140 kwa makosa mbalimbali ikiwamo kuvunja sheria za usalama barabarani.

Kamanda Bukumbi alisema kuwa bajaji hizo zilikamatwa kwa makosa ya kuzidisha abiria, kukiuka utaratibu wa leseni ya njia (routes), kutokuwa na leseni za udereva, kutokuwa na bima na kutokuwa na leseni za usafirishaji zinazotolewa LATRA.

Makosa mengine ni ubebaji wa mizigo na kuegesha maeneo yasiyoruhusiwa kwenye maeneo mbalimbali ya Manispaa ya Iringa, ambayo ni eneo la mzunguko Samora, mjini kati, Kihesakilolo, Mgongo na Ipogolo hadi Samora.

Kamanda Bukumbi alitoa wito kwa madereva na wamiliki wa vyombo vya moto kuhakikisha wanafuata sheria za usalama barabarani ikiwa ni pamoja na utii wa sheria bila shuruti, vinginevyo hatua kali zitachukuliwa dhidi yao, ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani.

# MAISHA

MACHI 5, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 13


**Mitindo mtandaoni**



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Namna ya kutumia kabati kama urembo wa nyumba



Ukurasa 12

**HARUSI**





## USO WENYE RAHA

# Njia za kuondoa ndevu, nywele

Ukurasa 14


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA





| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| T | R | A | ■ | I | T | V |
| A | ■ | ■ | ■ | K | ■ | U |
| M | ■ | B | A | A | ■ | M |
| B | A | I | ■ | T | A | I |
| I | ■ | N | A | E | ■ | L |
| K | ■ | G | ■ | ■ | ■ | I |
| O | G | O | ■ | L | O | A |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


BEE, PUA, AMA, OFA, NOA, TAA, BAA, NIA PAMBANO, AMKAMDE, TANGA AMANA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

JE, HUYU NI NANI? TUMIA PENSELI KUUNGANISHA NAMBA 1 HADI 21



## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA

SHUHUDIA jinsi mgambo walipokwenda kumkamata jamaa mmoja

**Mgambo:** Hodi, hodi
**Jamaa:** Kimya
**Mgambo:** Hodi, hodi wenye nyumbaa
**Jamaa:** We nani kwani?
**Mgambo:** Sisi mgambo
**Jamaa:** Sawa, mnataka nini?
**Mgambo:** Kuongea na wewe
**Jamaa:** Kuongea na mimi?!
**Mgambo:** Ndio
**Jamaa:** Mko wangapi?
**Mgambo:** Watatu
**Jamaa:** Kama mko watatu si muongee wenyewe...!!!

**SWALI**

Paka ana manufaa gani kwa binadamu?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Kwa nini usikilize zaidi kuliko kusema?

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vyetu vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki iliyopita nilizungumzia watoto wanaojikuta wakilelewa na wazazi wagomvi, wanaozozana kila mara tena mbele yao.

Wako baadhi ya wazazi hasa ambao ama wote wawili ni walevi wa pombe au mmoja wao. Vile pombe isivyo na aibu ikibugiwa kupita kiasi, ndivyo wanywaji wanavyojiachia kwa maneno makali vinywani mwao, mengine yasiyoweza kutamkika.

Watoto wanapoyasikia yakitamkwa na wazazi wao, huamini kwamba hata wao wakiyatamka hayana madhara. Kumbe ni bomu linalosubiri kulipuka baadaye. Nikasema wiki iliyopita kwamba maneno ni nguvu. Kile mtu anachotamka kiwe kizuri au kibaya, ndicho kitakachotokea.

Maneno yanaweza kujenga au kubomoa. Kinywa kikitamka laana inampata mlengwa na kikitamka baraka hali kadhalika inakuwa baraka kwa mhusika. Kwa mantiki hiyo, tunapaswa kuwa makini tunapotamka jambo na zaidi sana tujitahidi kujizuia.

Ni muhimu kujizuia kwa sababu hata Mungu ameliweka vema hilo pale aliposema kwenye neno lake kwamba, "Umetegwa kwa maneno ya kinywa chako mwenyewe, umekamatwa kwa maneno ya kinywa chako mwenyewe".

Hiyo ina maana katika kinywa kuna mtego, yapo maneno unaweza ukayaongea baadaye yakawa ni tanzi mbele yako. Yakawa ni mtego mbele yako. Mtu anaweza akajinenea kwamba mimi siolewi tena, yaani sitaki kuolewa.

Kiukweli utakaa usiolewe kwa sababu uliwahi kujitamkia kwa kinywa chako mwenyewe. Hujawahi kumsikia mtu akitamka, yule mimi nitamuua, nitamfanyia kitu kibaya yule. Sasa watu wabaya wakiyachukua maneno yale utashangaa kweli kitu kibaya kinampata mtu kama ilivyotamkwa. Mashuhuda nao watasema ni kweli fulani aliwahi kutamka atamfanyia kitu kibaya na imetokea vile vile!

Pia andiko lingine la Mungu linasema, "Atakayekupenda maisha na kuona siku njema, auzuie ulimi wake usinene mabaya na midomo yake isiseme hila". Kwa hiyo ili uwe na siku njema, ili uwe na mafanikio, ili uanze vizuri ni vema kuuzuia ulimi wako.

Pia anasema: "Anayezuia kinywa chake, huiponya nafsi yake". Nafsi yako inaponywa kutokana na wewe kujizuia. Mtu anaweza kujiuliza, je, kwa maana hiyo hata kwa maneno yangu ninayotamka yasiyofaa, mabaya, yananiumiza mimi mwenyewe katika nafsi?

Jibu: Yanaweza kukumiza kwani unaweza kutamka kitu, ukakumbuka kumbe ulikosea. Hapo nafsi yako inaanza kukosa raha, moyo wako unaanza kuugua, unajihukumu na kuanza kujisikia vibaya. Ndio pale mtu anaondoka kwenda kwa jirani yake na kumuomba amsamehe.

Unamwambia ni kweli ulimi uliteleza niliongea pale. Nafsi inaanza kujisikia vibaya, unakosa amani na kupata mahangaiko ya moyo. Kwa hiyo ni vizuri kujizuia ili tusiingie katika mitego mbalimbali.

Msomaji wangu, hebu sasa tuangalie nini kifanyike ili kuepusha balaa. Kwanza, anza kujizoesha kusikiliza zaidi kuliko kusema. Kabla hujasema kitu, hujatambua chanzo cha kitu, hujaijua habari vizuri usikimbilie kusema kwa sababu unaweza kukosea. Maana ulikuwa hujui.

Mtu anaweza kukuta mazungumzo naye akaingilia akaanza kuchangia utafikiri alikuwepo tokea mwanzo. Hata kwenye mabasi ya abiria utaona mtu anaingia na kuanza kuongea utafikiri alikuwepo. Akaanza hata kujiapisha kuwa asemacho ni hakika, vitu ambavyo hajawahi kuviona. Kwa hiyo tuanze kujizoesha kutumia masikio yetu zaidi kuliko kutamka haraka. Hiyo itatuponya nafsi na siku njema itaonekana katika maisha yetu.

Msomaji wangu, jambo ambalo sote kama wanadamu tunapaswa kutambua kwamba vinywa vyetu vinaumba. Kwa mfano, mtoto unaweza kumuumba kutokana na unavyoongea kwa kinywa chako. Hivyo yatupasa kuwa makini sana.

Neno la Mungu linasema, ni vizuri kunyamaza kuliko kusema wala kukasirika, tuzuie hasira. Lakini pia neno linasema muwe na hasira, lakini usitende dhambi, jua lisichwe bado uchungu vifuani mwenu haujawatoka.

Unajua mtu anakasirika lakini amenuna wiki nzima, jua linakuchwa linazama bado ameshikilia hasira. Hilo Mungu hapendi. Hivyo ni vema kuachilia kabla jua halijachwa. Angalia jua linapozama, ukijiona umekasirika, anza kumuomba Mungu akusaidie.

Hiyo ni kwa sababu uchungu una madhara. Unaweza kupata tatizo la moyo, vidonda vya tumbo, unaanza kukonda tu hujielewi, unapauka una mawazo, kisa una uchungu mtu fulani alikuumiza.

***Umeshaumizwa imetokea kama hawezi kukuomba msamaha, wewe jitahidi kuyaachilia ya ndani yafute yawe sifuri. Bila shaka umejifunza jambo hapo. Una kisa? Ujumbe 0715268581.***

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi



# Kusigina misingi ya kanisa hakutatuacha salama

BUSARA imeshinda! Subira, uvumilivu na usikivu umejenga mnara wa hekima. Ndivyo ninavyoweza kueleza kuhusu kazi kubwa inayofanywa kwa weledi mkubwa na Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Frederick Shoo.

Nianze na Kongole kwa Dk. Shoo na wanaomshauri juu ya utatuzi wa migogoro inayoitafuna KKKT. Migogoro mingi inayojitokeza ni ile inayotokana na mgongano baina ya watu, baada ya kutofautiana mawazo, mitazamo, uwajibikaji wa pamoja na mambo mengine yanayoweza kusababisha kutoelewana kuhusu jambo fulani.

Hali ya kutoafikiana au kukubaliana baina ya watu wawili au pande mbili, ndiyo huzaa migogoro tunayoiona sasa. Mingi ni ile ya kimaadili na kung'ang'ania madaraka, migogoro rahisi au inayoweza kuwa migumu kufanya utatuzi na ambayo inahitaji tahadhari, ni ile inayohusisha hitilafu za kimaadili au maslahi ya kanisa au mtu na mtu.

Katika utatuzi wake, mwafaka wa pande zote mbili unategemea mtu kujikosoa au kujirudi kimaadili, tendo ambalo huwa lina ugumu wa kinidhamu. Wakati wa utatuzi wake ni lazima ujitahidi kupima kwa hekima madhara ya migogoro inayochomoza kila mara na kuchukua tahadhari zote.

Uwezo wa Askofu Dk. Shoo katika utatuzi wa migogoro hauna shaka. Migogoro kadhaa aliyoibeba na kuimaliza, amekuwa akifanya uamuzi sahihi kwa busara na utulivu wa moyo. Tunakumuka busara aliyoitumia hadi kumaliza mgogoro uliokuwa umeota mizizi katika Dayosisi ya Konde ambayo iki katika mikoa ya Mbeya na Songwe.

Kupitia Halmashauri Kuu ya KKKT, aliunda kamati ambayo ilizikutanisha pande mbili zilizokuwa zikihusika na mgogoro na baada ya kushindwa kufikiwa mwafaka, kamati ilirejesha jambo hilo kwa Mkutano Mkuu Maalum wa Dayosisi ambaoulifikia uamuzi wa kupiga kura ya kutokuwa na imani na aliyekuwa Askofu, Dk. Edward Mwaikali na hatimaye kumchagua Mchungaji Geoffrey Mwakihaba kuwa Askofu wao.

Siku chache zilizopita, Askofu Dk. Shoo, aliumaliza mgogoro wa waumini wa KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki dhidi ya kiongozi wao, Askofu wao, Lucas Mbedule uliodumu kwa muda wa miaka sita. Mgogoro huo umefikia tamati baada ya Askofu Dk. Shoo, kukutana na viongozi wa Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Kanisa hilo mkoani Mtwara na kusuluhisha mgogoro huo kwa muda wa siku mbili.

Askofu Shoo amenukuliwa akisema Halmashauri Kuu ya Dayosisi ya Kusini Mashariki ya KKKT, imepokea na kuridhia ombi la kujiuzulu kwa Askofu Mbedule kama alivyoomba. Hata hivyo, Mbedule ataendelea kuhudumu kama Askofu wa Dayosisi hiyo mpaka utakapofanyika mkutano mkuu wa dayosisi Julai, mwaka huu, atakapochaguliwa askofu mwingine.

Hata Askofu Dk. Shoo mwenyewe amenukuliwa akisema migogoro ndani ya KKKT mingi inatokea pale taratibu za kiutumishi na misingi ya kanisa vinapokiukwa, Huko ndiko kunakoitwa kukanyaga au kusigina katiba ya kanisa. Hiyo inamaanisha kwamba baadhi ya wachungaji wa KKKT wamekuwa hawafuati taratibu za kikatiba za kuwa na mikutano. Matokeo yake ni migogoro kuibuka mara kwa mara. Ni dhahiri kuwa yako madhara makubwa ya kusigina misingi ya kanisa, ambako ni wazi kwamba hakuwezi kutuacha salama.

Ni ukweli usiopingika kwamba kuzuia migogoro ni kiini cha amani ya kudumu. Uwezo thabiti wa upatanishi na matumizi ya mbinu za utatuzi wa migogoro kwa njia ya kidiplomasia hujenga amani katika jamii kote ulimwenguni.

Ni vyema viongozi wetu wa kiimani, wakatafakari, wakahesabu gharama za migogoro kabla ya kuruhusu mizozo, kwa kuwa amani ya kudumu na endelevu, inataka kuwepo kazi thabiti na viongozi imara ili kujenga utulivu, ambao ni maendeleo jumuishi.

Achilia mbali katiba ya KKKT ambayo wengi hatujaiona, ukisoma ibara 107A (2) (d) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, inazungumzia kukuza na kuendeleza usuluhishi katika migogoro.

Ibara hiyo inaeleza pamoja na mambo mengine, njia mbadala ya utatuzi wa migogoro inayojumuisha utaratibu wa usuluhishi (arbitration), upatanishi (mediation), kurudisha mahusiano ya kirafiki (reconciliation) na mazungumzo kufikia makubaliano (negotiation).

Kwa hiyo, suala la tatuzi wa migogoro kwa njia mbadala ni takwa la Kikatiba. Njia hii ya utatuzi wa migogoro limehimizwa katika vitabu vya dini ambavyo wengi wetu ni waumini wake. Ni mpango wa Mwenyezi Mungu kuona watu wake wanatatua tofauti zao kwa njia ya usuluhishi.

Godfrey Mushi ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini.

***Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com Simu ya mkononi: +255 767 535490***

# HARUSI




Desemba 30, 2022 ilikuwa siku ya kukumbukwa kwa Gaudin Gration na Bibiana Deus baada ya kufunga ndoa takatifu katika Kanisa Katoliki la Katoke, Muleba mkoani Kagera na baadaye tafrija fupi iliyofanyika katika ukumbi wa Suzana.

# MITINDO







# Mitindo mtandaoni

SANAA ya mitindo ya mavazi ni miongoni mwa vitu vinavyosaidia vijana kujipatia ajira na kujiingizia kipato.

Vijana wengi kwa sasa wamehamasika na kuanza kujichanganya katika tasnia hiyo na hivyo kuondoa dhana kwamba sanaa hiyo hailipi.

Wakitumia teknolojia ya kisasa ya mawasialiano, watu wanakutanishwa katika majukwaa ya mitandao ya kijamii kujadili, kubuni na kufanya biashara ya mavazi.

Kimsingi mambo yamekuwa moto, kila aina ya mavazi unaweza kuona katika kiganja chako, unachotakiwa wewe ni kuuliza bei na kutoa oda na saa chache unajikuta unapata nguo mpya.

Kutokana na mabadiliko hayo, zipo changamoto ambazo zinaonekana kuwa kikwazo kwa vijana katika kujikomboa kiuchumi kupitia mitindo katika mitandao.

Mbunifu wa mavazi, Mustafa Hassanari , anasema kwa kutumia teknolojia ya kisasa mtu anaweza kubuni, kutangaza na kuuza kwa muda mfupi zaidi, tofauti na zamani.

Anasema kikwazo kikubwa katika soko la mtandaoni baadhi ya watu wanakuwa sio waamifu kwa kuuza mavazi tofauti na mteja alivyoagiza au nguo kukosa ubora unaokubalika.

Hata hivyo anathibitisha kwamba soko la mitandaoni limekuwa kubwa na linasababisha hata wabunifu kupata wakati mgumu wa kutengeneza nguo zinazoendana na wakati uliopo.

UREMBO



USO WENYE RAHA

# Njia za kuondoa ndevu, nywele

LEO kwenye urembo tutaongelea jinsi ya kuondoa nywele za usoni pamoja na ndevu ambazo siku hizi wanawake wengi wamejikuta kuwa nazo.

Kwa kutumia kiwembe ni rahisi sana kwa sababu ni kitu cha dakika, lakini ujue nywele hizo zitaota haraka.

Hapa nimekuletea vitu asilia ambavyo vinaweza kukuondolea nywele hizo na ukakaa kwa muda mrefu bila kuziona na usipate madhara ya mapele kama ambavyo ungenyoa na kiwembe.



**Mahitaji**

Vijiko viwili vya asali, kijiko kimoja cha ngano na vijiko viwili vya juisi ya limao.

Chukua ngano isage mpaka upate unga wake. Changanya na asali pamoja na limao, baada ya hapo paka kwenye eneo lenye nywele.

Ukimaliza acha kwa muda wa dakika 15, kisha osha na maji ya vuguvugu.

Baada ya hapo paka kipako chako rudia kupaka mchanganyiko huu mara mbili mpaka tatu kwa wiki ndani ya mwezi mmoja utaona nywele hizo zimepotea kabisa.

Kama una ngozi laini isiyotaka mikikimikiki jaribu kidogo ili isije kukuletea matatizo.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Ndizi mbivu, nazi inavyonoga

WENGI tumezoea kupika ndizi mbichi aina ya mshale, mzuzu na Bukoba, lakini leo tunaelekezana tofauti kupika ndizi mbivu na nazi.

**Mahitaji**

Ndizi mbivu 10 aina ya mzuzu, nazi kavu tatu, sukari kiasi na hiliki kiasi.

Menya ndizi zako kwa kuzipasua katikati kwa marefu, ukiziondoa taratibu ndani ya ganda lake.

Zimenye kisha maganda uyaoshe. Yapange vizuri maganda hayo ndani ya sufuria safi (kwa chini). Chukua vipande vya ndizi uvipange juu ya maganda.(ndizi ziweke chali, usizifunike).



Kuna nazi uchuje tui zito na jepesi utenge. Chukua tui jepesi ulitie katika ndizi kisha uziache. Zipike mpaka tui likauke na ndizi ziive. Nyunyizia sukari kidogo. Twanga hiliki utie juu yake.

Chukua lile tui zito ulimimine uache liwe linatokota kwa moto mdogo sana.

Tui likikauka na kutoa mafuta epua na uziache zipoe. Unapopakua, zitoe taratibu bila ya kuzivuruga.

## MAISHA NI NYUMBA
Na Restuta James

# Mbao, mrunda unavyokuwa pambo nyumbani

WIKI iliyopita tuliona namna ambavyo mapambo ya asili kama batiki au ukili yanavyoweza kubadilisha mwonekano wa nyumba na kuifanya ivutie.

Leo tutaona namna ambavyo vitu vinavyoonekana vya kawaida vinavyoweza kubadilisha mandhari ya nyumba.

Wataalamu wa mapambo ya ndani wanaeleza kuwa kila mazingira mtu anayoishi yana vitu vinavyoweza kubadilishwa kidogo tu na kuwa pambo la nyumba.

Wanaeleza kuwa vitu kama ubao au mrunda uliotumika au mpya vinaweza kukupunguzia bajeti yako ya mapambo kama utaviongezea ubunifu 'kidogo.'

Mbali ya malighafi hizo zinazoweza kupatikana kiurahisi, wataalamu hao wanasema mtu akiwa na nia ya kubadili mwonekano wa nyumba anaweza kununua rangi aina mbili au zaidi na kupata ukuta kwa michoro ambayo angeitaka na nyumba ikaonekana nzuri.

Wakianza na mbao pamoja na mrunda au mti mwingine, mwenye nyumba anaweza kukata urefu au umbo analotaka na kupaka rangi za kuvutia kisha akatumia kama pambo chumbani au sebuleni.

Unaweza pia kutumia kipande cha mbao na kukinakshi kwa rangi uipendayo halafu andika maneno mazuri kwa kutumia rangi nyingine.

Kwa kuwa kazi hiyo unaweza kuifanyia nyumbani, unaweza kuandika maneno ya upendo ukayaweka kwenye chumba cha watoto au neno la kumkaribisha mgeni na kuweka kwenye ukuta wa varanda yako.

Wataalamu hao wanaeleza kuwa aina hii ya mapambo yanafaa kubuniwa kwa ajili ya kuweka sebuleni, vyumba vya wakubwa na hata kwa watoto.





# Namna ya kutumia kabati kama urembo wa nyumba

KABATI la vyombo ni miongoni mwa samani zenye uhitaji mkubwa kwenye nyumba.

Watu waliobarikiwa kujenga au kuishi kwenye nyumba yenye nafasi ya kutosha, kabati huwa moja ya vitu muhimu kwao kwa ajili ya kuhifadhia vyombo.

Lakini leo nataka tuzungumzie kazi nyingine ya kabati kwenye eneo la urembo kwenye nyumba.

Kama ilivyo urembo mwingine kwenye nyumba, kabati la vyombo nalo lina nafasi ya kutumika kama urembo.

Kutumika kwa kabati kama urembo si kwa kuweka maua au urembo mwingine ndani yake ni kwa kutumia vyombo hivyo hivyo ambavyo badala ya kutumika kwa ajili ya matumizi ya chakula, pia vitumike kama urembo.

Na ili vitumike kama urembo, kitu cha kwanza lazima kwanza tujue eneo linapopaswa kuwekwa ndani ya nyumba husika.

Jambo lingine lazima kuhakikisha kwamba vyombo vinavyowekwa kabatini ni vile vyenye mvuto au vizuri, usichukuea tu vyombo ilimradi na kwenda kuviweka humo.

Hakikisha unazingatia rangi za vyombo vyako vinavyowekwa kabatini, zisiwe zile za kuumiza macho sana na ikiwezekana rangi zake zisipishane sana na zile za vitu vyote vilivyopo kwenye nyumba yako.

Kuwa mbunifu kuvipangilia kwenye kabati ili vilete mvuto, zingatia aina na muundo wa vyombo. Kama ni sahani, hakikisha unapangilia kuanzia zile kubwa






kuelekea ndogo zake, fanya hivyo na kwa glasi, vikombe, bakuli na vinginevyo ambavyo ni vizuri unavyokuwa umeviandaa kwa ajili hiyo.

Kumbuka si lazima viwe vinatumika, vinaweza kuwa maalumu kwa urembo tu na vile vya kutumia ukaviweka sehemu nyingine au katika kabati la juu la jikoni.

Na kama uwezo hautoruhusu, unaweza pia ukavitumia, lakini unapomaliza unahakikisha kwamba unavisafisha vizuri na kuvirudisha katika sehemu yake vinapopangiliwa na katika hili ubunifu zaidi unahitajika.

Katika mpangilio unaweza kuamua glasi zikae sehemu yake, au ukaamua kila shefu zikae tatu au nne kwa mpangilio mzuri, au kila aina ya chombo ulichonacho ukakitumia kwa mpangilio maalumu katika shefu zote ili 'kunogesha zaidi'.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
FURSA
HA HAAA! HA HA HAAAA! HA HAA!
ULEVI
UJASIRI-AMALI
VIJANA
KUSIKOJULI-KANA
UTOPOLO WOTE NINAO-UFANYA BAR TUKIWA NA WEWE BWASHEMEJI MKE WANGU ANAUJUA!
SIO UTOPOLO TU, ATAJUA HADI UKOLO UNAOTAKA KUUFANYA BAR
DALADALA NI "KAMA MAJI" MMEWEKEWA MWENDO KASI NA TRENI, LAKINI MNAVIKIMBIA! MNAKUJA KWENE STAREHE
HUJUI UNENALO! SISI TUNAKUSAIDIA USIRUDI KIJIJINI NA FAMIALIA YAKO
STAREHE KWANI KUNA KASINO HUMU?!
BAHATI YAKO NIPO SITI YA NYUMA, SIVYO MAJI UNGEITA MMA!!!
TENA HAWA WAKIKOSA KAZI WANAHAMIA KWENYE KABALI!
FALA HUYU!
ACHA NYODO!
SA'MBONA MKALI KISA KUKUULIZA DODOMA LINI?!
NATAKA UELEWE SIO KILA MTUMISHI NI WA SIRIKALI, SISI WENGINE NI WATUMISHI WA "MUNGU"
KUDAI TALAKA NI RAHISI SANA LAKINI SASA KIFUATACHO!
'MADANGA'
BABA MKWE NATAKA KUMRUDIA MKE WANGU UNASEMAJE?
NASEMA KAMA MTU AKIFA ANARUDIA KUISHI NJOO TU.
HILI NALO NENO!
JIFUNZE KUONGEA LUGHA
SHOGA ETI MUMEO JANA KANAMBIA ANANTAKA!
MKUBALIE... MI'MWENYEWE ALIKUWA MUME WA SHOGA'ANGU
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...UNAGOMBEA MSIBA KUUGUZA UJAONEKANA

**HABARI KIMATAIFA**

## Mama aliyeua watoto watano, auawa baada ya kuomba kuuliwa

**BRUSSELS,** UBELGIJI

MWANAMKE mmoja raia wa Ubelgiji ambaye aliwaua watoto wake watano, hatimaye ameuwawa baada ya ombi lake la kuuliwa kukubaliwa.

Genevieve Lhermitte, alimuua mwanawe wa kiume na binti zake wanne, wenye umri wa miaka mitatu hadi 14, miaka 16 iliyopita katika mji wa Nivelles, wakati baba yao hayupo.

Baada ya kufanya mauaji hayo, alijaribu kujitoa uhai lakini akashindwa, na baadaye alipiga simu ya dharura ya polisi.

Mama huyo mwenye umri wa miaka 56 alihukumiwa kifungo cha maisha jela mwaka wa 2008, kabla ya kuhamishiwa katika hospitali ya magonjwa ya akili 2019.

Nchini Ubelgiji sheria inaruhusu watu kuchagua kuuawa ikiwa watachukuliwa kuwa na matatizo ya kisaikolojia yasiyovumilika na mateso ya kimwili, ambayo hayawezi kuponywa.

Hata hivyo, mtu lazima awe na ufahamu wa uamuzi wake huo na aweze kuelezea matakwa yake kwa njia ya busara na thabiti.

"Ni utaratibu huu maalum ambao Lhermitte aliufuata, huku maoni mbalimbali ya kimatibabu yakiwa yamekusanywa," wakili wake alisema.

Mwanasaikolojia Emilie Maroit, aliambia idhaa ya RTL-TVI kwamba Lhermitte alichagua kufariki Februari 28, kama ishara ya kuheshimu watoto wake.

"Huenda pia ilikuwa ni kwa ajili yake kumaliza kile alichoanza, kwa sababu kimsingi alitaka kukatisha maisha yake siku ambayo aliwaua watoto wake," mwanasaikolojia alisema.

Mauaji ya watoto hao watano yalifanyika 2007, na kesi yake ilifuatiliwa na idadi kubwa ya raia wa nchi hiyo.

Wakati wa kesi, mawakili wa Lhermitte walidai kwamba alikuwa amechanganyikiwa kiakili na hapaswi kupelekwa gerezani.

Lakini mahakama ilimpata na hatia ya mauaji ya kukusudia na kumhukumu kifungo cha maisha jela.

Mnamo 2010, Lhermitte alifungua kesi ya madai ya euro milioni tatu kutoka kwa daktari wa akili wa zamani, ambaye alidai kutochukua hatua stahiki na ndio chanzo cha kutofanikiwa kuzuia mauaji hayo.

Hata hivyo, aliachana na kesi hiyo baada ya miaka 10.

Tangu 2014, Ubelgiji imeruhusu watoto kusaidiwa kufa pamoja na watu wazima, ikiwa ni wagonjwa mahututi na wana maumivu makali na ikiwa wana idhini ya wazazi.

# Rais Biden aondolewa uvimbe wa saratani

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, ameondolewa uvimbe kwenye ngozi wenye saratani mwezi uliopita baada ya kufanyiwa uchunguzi wa kawaida wa afya.

Taarifa ya Ikulu ya White House, ilisema tishu zote za saratani ziliondolewa na hakuna matibabu zaidi yanayohitajika.

Daktari wa Rais Biden, Kevin O'Connor, alisema kiongozi huyo ataendelea na uchunguzi wa ngozi kama sehemu ya huduma yake ya afya inayoendelea.

Rais huyo mwenye umri wa miaka 80, alifanyiwa uchunguzi wa mwili mwezi Februari mwaka huu, na kubainika ni mzima na anafaa kufanya kazi zake.

O'Connor, aliandika barua iliyotolewa kwa vyombo vya habari juzi kwamba uvimbe huo uliondolewa kwenye kifua cha Biden tangu Februari 16, katika Kituo cha Kitaifa cha Matibabu cha Kijeshi cha Walter Reed nje ya Washington DC.

"Hakuna matibabu zaidi yanayohitajika, eneo hilo limepona vizuri tangu kufanyiwa matibabu," alisema daktari huyo.

Ujumbe huo ulisema kwamba aina ya saratani iliyopatikana inafahamika kama basal cell carcinoma' na kwa kawaida haisambai.

Januari mwaka huu, mke wa Biden, Jill Biden, aliondolewa uvimbe sehemu tatu, na mbili kati ya hizo ilipatikana na seli za saratani ya basal.

Madaktari wanashauri kwamba njia bora ya kuzuia saratani ya ngozi ni kufunika na kupaka mafuta ya kuginga mionzi ya jua, hata wakati wa baridi.

Rais Biden kwa muda mrefu amekuwa mtetezi hodari wa kupambana na ugonjwa wa saratani.

Mtoto wao mkubwa, Beau, alifariki 2015 kutokana na saratani ya ubongo.

Rais Biden anatarajiwa kutangaza kuwa atawania muhula wa pili madarakani hivi karibuni.

**BBC**



Mwanamke akiwa ameketi mbele ya hema kufuatia tetemeko kubwa la ardhi lililotokea wilaya ya Iskenderun nchini Uturuki, Machi 1, 2023. Zaidi ya watu 50,000 walikufa na maelfu ya wengine kujeruhiwa. **PICHA: EPA-EFE**

# Ukraine yazima mashambulizi

**KYIV,** UKRAINE

IDADI kubwa ya makombora yaliyoshambulia eneo la mashariki mwa Donetsk, yamefanikiwa kuzimwa na jeshi la Ukraine.

Vikosi vya Russia vilidai kuwa wanakaribia kuteka mji wa mashariki wa Bakhmut ambao ni kitovu cha mapigano makali kwa miezi kadhaa.

Mkuu wa jeshi la kibinafsi la Russia la Wagner, alidai eneo hilo limezingirwa na njia chache za kutoka ndio zimeachwa. Hata hivyo, Marekani imeahidi kutoa dola milioni 400 katika msaada wa kijeshi kwa Ukraine ili kuongeza hifadhi ya silaha za nchi hiyo zilizopungua wakati wa vita vyake vikali vinavyoendelea.

Waziri wa Mambo ya Nje, Antony Blinken alisema msaada huo ni pamoja na roketi za usanifu za Himars na howitzers ambazo Ukraine inatumia kwa ufanisi. Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky, alisisitiza kwamba vifaru na makombora yanahitajika ili kukomesha uvamizi wa Russia.

Marekani pia inatuma madaraja ya kimbinu kabla ya mashambulizi yanayotakiwa na Ukraine.

Kutolewa kwa vifaa hivyo vinavyoruhusu magari ya kivita kuvuka mito na mitaro kunakuja huku maafisa kadhaa wa kijeshi wa Ukraine na wataalam wakipendekeza operesheni hiyo inaweza kuanzishwa katika wiki zijazo.

Wakati huo huo, Russia siku ya Ijumaa iliendeleza mashambulizi yake dhidi ya mji wa Bakhmut, huku wapiganaji wa Wagner wakidai wameuzingira mji huo.

Katika taarifa iliyotolewa jana, jeshi la Ukraine lilisema wanajeshi wa Russia waliendelea na juhudi zao za kuuzingira mji huo, lakini mashambulizi mengi yalizimwa kabla kufika mahali yalipolengwa.

Watu waliamriwa kuhama makazi yao katika mji wa kaskazini-mashariki wa Kupiansk, mkoa wa Kharkiv, baada ya mashambulizim kuwa makali.

Mamlaka za eneo zilisema familia zilizo na watoto na watu ambao wanaweza kuhamia sehemu zingine, walipaswa kuondoka kwa sababu ya kuongezeka kwa mashambulizi ya mara kwa mara kutoka kwa wanajeshi wa Russia. **BBC**

MAKALA

# ZUNGUMZA USIKAE KIMYA



Na Magabilo Masambu

WAANDISHI na wataalam mbalimbali wa fasihi wamekuwa wakihusisha migogoro katika jamii kama sehemu ya maisha na kwamba jamii isiyo na migogoro imekufa. Maana yake ni kwamba hakuna siku tutaishi bila migogoro ambayo inaweza kuwa ya binafsi, mtu na mtu, watu na taasisi na kadhalika.

Migogoro baina ya watu na taasisi mara nyingi haisababishi matatizo makubwa kwa sababu ni ya wengi. Migogoro binafsi ni hatari zaidi katika maisha. Wazungu wanaita "self conflicts". Ni kati ya migogoro mibaya zaidi na imeangamiza watu wengi sana. Leo nataka nikueleze njia rahisi ya kutatua ili kuepukana na madhara makubwa yanayoweza kukupata na wakati mwingine kusababisha hata mauti.

Ukichunguza baadhi ya magonjwa mengi siku hizi hata vyanzo vyake, baadhi hushindwa kugundulika kitabibu lakini watu wanaendelea kuangamia. Magonjwa waliyougua watu wenye makamo fulani, siku hizi anaugua kila mtu. Magonjwa ya presha na sukari zamani yalionekana magonjwa ya matajiri lakini siku hizi hata watu wasio na pesa wanaugua!

Ugonjwa wa vidonda vya tumbo sasa umekuwa kama malaria. Kila mtu anakwambia anaumwa vidonda vya tumbo yaani imekuwa fasheni na kama huugui vidonda sasa kuna uwezekano wa watu kushangaa. Natambua kwamba pamekuwa na mabadiliko makubwa sana ya kimaisha na hii ni kwa sababu ya mabadilikio ya hali ya hewa ambayo kwa kiasi kikubwa, yamesababishwa na shughuli zetu za kibinadamu kwa sababu ya ongezeko la watu. Tunahitaji maeneo ya kuishi lazima tukate miti tujenge. Uharibifu wa vyanzo vya maji, jambo linalosababisha tusizalishe chakula cha kutosha, hivyo kuwa na matatizo makubwa ya njaa na maisha kuwa magumu.

Nyumba ikikosa chakula maana yake fedha nyingi hutumika kukinunua chakula. Kwa maana hiyo inabidi tufanye kazi kwa ajili ya kununua huku mambo mengine yakisimama. Watoto wanahitaji ada na fedha hatuna. Tunapata migogoro binafsi ambayo inasababisha migogoro ya familia na mwisho wa siku tunagombana na kuvunja familia.

Migogoro binafsi huwezi kupata tiba ya dawa na dawa yake kubwa ni ushauri kutoka kwa watu sahihi. Lakini tiba kubwa zaidi ni kukubaliana na hali jambo linalowashinda wengi. Jambo la kukubaliana na matatizo ni jambo gumu sana kwa watu wengi. Wanaojinyonga au kunywa sumu kwa sababu ya matatizo ni kukosa uwezo wa kukubaliana nayo. Wanaougua vidonda vya tumbo kwa kuwaza wanashindwa kukubaliana na hali za matatizo walizo nazo. Njia bora kabisa ya kukubaliana na matatizo ni kupata ushauri sahihi.

Ushauri huu mara nyingi ukitoka kwa watu wenye uzoefu wa matatizo kama yako na namna walivyoyatatua, husaidia zaidi kwa sababu unaweza kupata ushauri juu ya tatizo ambalo uliliona ni kubwa, kumbe wenzako wanayo makubwa zaidi. Utapataje ushauri huku ukiwa kimya? Ni wazi kwamba hakuna ajuaye awazalo mtu ni mpaka pale utakapolitoa.

Tunasema tunayofikiri, hatufikiri tunayosema. Huwezi kunyamaza nikajua unafikiri nini japo unaweza kuiona tofauti hata kama hujasema chochote. Ndiyo maana unaweza kusikia mtu anakuuliza mbona kama hauko sawa, mara nyingine utakubali, lakini wengi wanakataa na kutafuta furaha ya bandia kitu ambacho ni hatari sana kwa maisha yao. Ukiwa na tatizo na mtu akagundua mwambie ukweli kwamba ndiyo kuna jambo linanisumbua kama unamwamini pia.

Wako wanaosema ushauri wa matatizo lazima kuwaona wataalam. Ni kweli lakini mtaalam wa kwanza ni mwenye uzoefu katika jambo lenyewe. Anaweza akose njia sahihi ya kukushauri lakini utakuwa umepata mwanga ikiwa yeye alilishinda kwa njia bora. Ushauri uwe umetoka kwa mtaalam au kwa mtu mwenye uzoefu kazi inabaki kwako wewe unayeshauriwa kuchagua upande utakaokupa nafuu ya moyo. Mtaalam na mwenye uzoefu wote ni binadamu wanapitia matatizo yale yale, kwa hiyo ni muhimu kuchuja japo kwa kulisema tu tatizo lako utakuwa umelitatua kwa kiwango fulani.

Ukitaka kuishi kwa raha lazima uwe na mtu katika maisha yako unayeweza kuwa unamwambia yanayokusibu. Anaweza kuwa rafiki, ndugu wa aina ya rafiki au mtu yeyote wa karibu ambaye unaamini ukimwambia jambo halipeleki kwa wengine, bali atakusaidia kukushauri na yakaishia hapo.

YaKo matatizo ya ndoa, uchumi, uhusiano nje ya ndoa na maisha tu kwa ujumla. Ukikosa mtu wa kumshirikisha haya uko kwenye hatari kubwa ya kuchukua uamuzi mgumu ambao kila mmoja atayashangaa na ambayo yanaweza kuleta majuto makubwa maishani mwako.

Yako mambo ambayo yanaonekan ni ya aibu na kwamba nikimwambia fulani atanionaje. Kama unamwamini mwambie kisha utakuja kuona kumbe ni jambo dogo. Zungumza usinyamaze maana matatizo hayo yatakunyamazisha. Wanaume ndio waathirika wakubwa kuliko wanawake. Wao wanazungumza sana, ndiyo maana hata maisha yao ni marefu. Magonjwa kama vidonda vya tumbo yanawathiri zaidi wanaume kwa sababu ya kujiona miamba wa matatizo na kwamba nitakufa kiume. Hakuna cha kufa kiume badala yake utakufa na kuacha familia inahangaika. Usikubali zungumza mwanakwetu utapotea mara moja.

Ni muhimu kutambua kwamba matatizo ni sehemu yetu nasi ni sehemu ya matatizo. Hakuna maisha bila matatizo ndiyo maana vitu mbalimbali vinagunduliwa ili kutatua changamoto za matatizo yanayojitokeza. Watu walipotembea sana kwa mguu wakagundua baiskeli, baadaye wakaona hawafiki haraka wakatengeneza gari na kadhalika. Kwa hiyo tuyazoee lakini tutafute njia rahisi ya kuyatatua.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kesi ya khanga ya Monica aliyekimbilia Zambia na treni ya mizigo kukwepa jela*



Na Adam Fungamwango

HAPANA shaka kuwa wakati dunia ikisonga mbele pamoja na maendeleo ya kiuchumi, elimu na teknolojia, wanawake wamepiga hatua kubwa mno kwenye miaka ya hivi karibuni.

Wanawake wameonekana kuwa na maendeleo zaidi kwenye kila nyanja, kwenye elimu, uchumi, na uongozi, kiasi kwamba wengi wao wamekuwa viongozi kuanzia kwenye familia hadi taifa.

Wametoka kwenye mikono au minyororo ya kukandamizwa na wanaume, kuwategemewa wao kwa zaidi ya asilimia 90. Sasa wako kila sekta.

Wanawake wengi wao wamekuwa na uchumi mkubwa zaidi kuliko baadhi ya wanaume.

Kwa sasa wengi wao wamesoma, tofauti na wakati huo walikuwa wakiachwa tu nyumbani wapike chakula, na wanapokuwa wasichana wakubwa wanafundishwa jinsi ya kumtumikia mume, kabla ya kuolewa.

Mambo yamebadilika, kwa sasa wala si ajabu kumkuta mwanamke amejenga nyumba, amenunua gari, ana kazi yake nzuri, mfanyabiashara mkubwa, au hata ndogo ndogo, lakini inamfanya aishi vizuri kwa amani na utulivu. Ingekuwa ajabu ya mwaka hilo miaka ya nyuma.

Kuna mtu mmoja aliniambia huenda wanawake wengi nchini ndiyo wana magari ya kwao binafsi kuliko wanaume kwa sasa.

Anasema kwenye miji mikuu hivi sasa wanawake wengi wanaendesha magari, na mara nyingi ni ya kwao binafsi, tofauti na wanaume ambao wengine ni wafanyakazi, na baadhi wanaazima.

Wanawake kwa sasa wanawatunza mpaka wapenzi wao, au waume zao. Hiki ni kipindi ambacho tumeshuhudia wanawake wakipambana na maisha, lakini baadhi ya wanaume hasa vijana wamekuwa wavivu kupindukia, 'mabishoo', waonachagua kazi, vivyo baadhi yao wanatunzwa na wanawake. Kuna wanaotunzwa kwa muda wakati hawana kazi, lakini wapo ambao hizo ndizo tabia zao.

Hata baadhi ya ndoa kutokaa muda mrefu na kuvunjika kwenye miaka ya karibuni ni kwa sababu ya kutojitambua kwao.

Mwanamke wa sasa hawezi kukaa kwenye 'ndoa ndoana' kwa sababu yeye mwenyewe anajishughulisha, tofauti na akinamama wa zamani ambao walikuwa wakivumilia ukatili, manyanyaso, shida, mateso kwa sababu ya kile walichokuwa wakikisema, "kama nikiachwa nitakwenda wapi?" Hakuna pa kwenda, atarudi tu nyumbani kwao, labda apate tena bahati ya kuolewa tena.

Hawakuwa wanajishughulisha. Kila kitu walimtegemea mwanaume.

Tunawatakiwa kila la kheri wanawake wote nchini, ambao wataungana na wenzao duniani kote kuadhimisha siku ya wanawake duniani Jumatano ijayo, Machi 8.

Hata hivyo bado wamebaki wanawake wachache ambao bado wana mitazamo ile ile ya kizamani. Hivi sasa kuna taasisi za mikopo na vikundi vya kukopesha ambavyo huvitumia kukopa kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

Wengine wamekuwa wakivitumia vizuri, lakini baadhi wamevitumia vibaya kiasi cha kujiletea matatizo makubwa wao wenyewe na familia zao.

Wamekuwa wakikopa na kushindwa kurudisha mikopo hiyo, hivyo kukombwa samani za ndani na mali nyingine walizonazo.

Tatizo ni kwamba wengine wanakopa bila ya kuwa na biashara yoyote. Wapo wanaokopa kwa ajili ya kuanza kufanyia biashara.

Hili ni kosa, mkopo mzuri ni ule wa kuendelezea biashara ambayo tayari unayo na inafanya vizuri.

Jiepushe kukopa halafu ndiyo unaanza kuwaza biashara gani ufanye. Sasa baadhi ya kinamama, hasa wale wa uswahilini.

Wao wanakopa kwa sababu ya kufanya sherehe za kutunzana, pati zisizo na kichwa wala miguu. Mtu anakupa ili anunue kabati, madera, vijora kwa ajili ya kwenda kumtunza mwenzake. Huyu hawezi kurejesha marejesho kamwe na yatamkuta ya kumkuta.

Mwanzoni mwa mwaka 1990, marehemu Freddie Ndala Kasheba akiwa na ameshatoka Orchestra Safari Sound (OSS) na kuunda kundi ya Zaita Musica waliokuwa na mtindo wa 'Zuke Moselebende', aliliona hili na kulitungia wimbo ulioitwa 'Kesi ya Khanga.'

Ni wimbo unahusu kisa cha mwanamke mmoja aliyekopa doti kumi za khanga, lakini akashindwa kulipa. Sasa sijui alikopa ili akauze kwa bei ya juu kidogo na yeye ajipatie faida, zilikuwa za kuvaa, au alikwenda kumtunza shoga yake kwenye kigodoro.

Hakuwa na kazi yoyote masikini, alipoona siku ya kulipa imefika alitoroka nyumbani kwao. Akaona hata hii haitoshi, akakimbia kabisa nchini, akaenda Zambia, tena kwa kudandia treni ya mizigo, maana aliona ya abiria ama siku ya kuondoka kwake ilikuwa baada ya tarehe ya marejesho, au aliona wanaweza kumkamata. Alifanikiwa kwa hilo. Lakini huku nyuma, akamuacha shoga yake ambaye alimuwekea dhamana alipokuwa anakopa. Huyu ndiye aliyepata msukosuko. Akakamatwa, akaswekwa rumande. Baadaye akaachiwa kwa dhamana kwa sharti la kumleta mdaiwa.

Bibie akaona isiwe tabu, alichoamua ni kufunga safari kwenda nchini Zambia kumsaka Monica ambako anasikia amekimbilia ili kikombe kimuepuke. Huu ndiyo wimbo wenyewe.

"Mama nipe nauli nikamfuate Monica, amekimbilia Zambia na treni ya mizigo ee. Kisa cha kukimbia madeni yamemzidi, doti kumi za khanga alizokopa hajalipa ee. Anatafutwa na polisi popote apatikane, na mimi rafiki yake nipo nje kwa dhamana eee.

"Nililala rumande siku mbili kituoni, usumbufu nilioupata kwa kweli sina raha ee.

Naona bora niende Zambia niende Zambia nikamtafute Monica, nimlete Dar es Salaam apambane na kesi yake, ooo Monica, ooo uko wapi eee.

Mahakamani wameshapanga siku ya kusikiliza kesi, alipofika nitapelekwa jela kutumikia kifungo ooo Monica, eee uko wapi eee."

Hili ni funzo, hasa kwa akinamama. Unatakiwa kukopa kwa malengo. Na wale wanaowawekea dhamana nao wanatakiwa wawe waangalifu. Mtu anakwambia tu nidhamini na wewe unakubali bila kumfahamu vizuri au tabia zake kwa undani ni hatari kubwa.

**Tuma meseji 0716 350534**

HADITHI

HAKUNA aliyeamini alichokisikia, wala aliyeamini macho yake kwa kile alichokiona. Awali kulikuwa na vigelegele, ngoma, bashasha na furaha tele kwa watu wote waliohudhuria harusi hiyo. Bwana harusi Jerry Mohamed aliliongoza kundi la ndugu, rafiki na jamaa kutoka Dar es Salaam kwenda Kibaha kwa Mathias mkoani Pwani kwa ajili ya kufunga ndoa na mwanamke Vayajo waliyekubaliana kuoana. Mabasi, magari, bajaj, bodaboda, vyote vilimiminika kwenda huko kila mmoja akiwa na furaha tele. Kilichotokea ndicho kilicholeta mkasa mzima kwenye sakata hili la aina yake. Nini kimetokea? Kwa nini? Sababu ni nini? Na baada ya hapo nini kinaendelea? Kila nakala yako ya Nipashe itakupa majibu ya kisa hiki cha kushangaza.

# Harusi Imevunjika-21

Na Adam Fungamwango

(0716 350534)

"Ni kwamba tuliwakamata watu kadhaa, akiwemo mwanaume aliyekuwa anaishi naye anaitwa Jaziru kwa tuhuma hizo."

"Mhh, bado sijakuelewa afande, mwanaume aliyekuwa anaishi na huyu dada, wapi Dar es Salaam?"

"Ndiyo, wakati tunamkamata mhalifu Jaziru, tena nyumbani kwake tulifika saa nane za usiku, tulimkuta huyu dada na akajitambulisha kama mke wa mtuhumiwa."

Jerry kwa mbali alianza kufunguka macho. Alianza kuhisi kuwa huenda Vayajo siku ya harusi alipotoroka, alikimbilia kwa mwanaume huyu anayemsema afande. Akauliza tarehe ambayo alikamatwa huyo mtuhumiwa. Alipojibiwa akapata uhakika kuwa ni kweli Vayajo alikimbilia kwa mwanaume ambaye ndiyo huyo aliyekamatwa kwa wizi na utakatishaji pesa.

Kwa upande wake hata alipotorokwa hakutaka kuhisi atakuwa ametorokea wapi. Hakujisumbua wala kujidanganya kuwa atakuwa amekwenda kuishi kwa marafiki zake wa kike, au kwenda sehemu kufanya biashara. Alichodhani ndicho hicho hicho ambacho sasa kinabainishwa na afande.

"Kifupi tu ni kwamba huyu dada alikuwa anaishi na mwanaume Dar es Salaam anayeitwa Jaziru. Huyo jamaa na wenzake waliiba pesa nyingi na kuzitakatisha. Tuliwakamata kama nilivyokwambia tulimkuta huyu dada. Tulimuacha pale kwa sababu sisi tulimhitaji mtuhumiwa tu. Lakini baada ya uchunguzi, tukagundua kuna miamala ya pesa kutoka kwenye akaunti ya mwanaume wake kwenda kwake kiasi cha Sh. Milioni 10, ambazo zilitumwa kwa nyakati mbili tofauti. Awali zilitumwa Sh. Milioni saba, na baadaye tatu. Kama nilivyokwambia hizo zote ni pesa za wizi na utakatishaji, kwa sababu watuhumiwa hao wapo rumande, tumekuwa tukiwakamata watu wote ambao akaunti zao zilikuwa zinaingiziwa pesa na watuhumiwa. Tunafanya hivyo kwa ajili ya mahojiano, uchunguzi na kujiridhisha ili kukusanya taarifa zote, kuzichakata na kuchuja nani alihusika na nani hakuhusika. Kama ziliingizwa tu kwake lakini hakuhusika, basi atakuwa hana kesi ya kujibu, tutamrudisha sisi wenyewe, lakini kama atakuwa ameshirikiana na mwanaume wake basi atapanda mahakamani."




Mambo yamekuwa makubwa. Kila kitu kilimshangaza Jerry. Tarehe aliyotajiwa na askari ambayo Vayajo aliingiziwa pesa, ilikuwa ni ile ambayo alimtoroka na kwenda kusikojulikana.

Angejua kuwa zile Sh. Milioni saba za mwanzo alizoingiziwa na Jaziru, ndizo zilizomtia uchizi na kuamua kutoroka muda mfupi tu kabla ya kufunga ndoa!

Sasa ndipo Jerry alianza kutambua kuwa kukimbiwa kule kulichangiwa kwa asilimia kubwa na pesa zile za wizi na utakatishaji kutoka kwa mwanaume mmoja asiyemfahamu, anaitwa Jaziru. Siri sasa ilikuwa imefichuka.

Hapo hapo akakumbuka kuwa muda mchache tu uliopita wakati anambembeleza warudiane, Vayajo alimwambia ana kiasi cha pesa Sh. Milioni 10 benki, akiahidi kumpa wafanyie biashara akawa anajiuliza amezipataje? Sasa amepata jibu.

"Kwa hiyo hizo pesa itakuwaje?" Akauliza Jerry.

"Zitarudi mikononi mwa serikali, siyo za huyu dada, zote hata za hao watuhumiwa."

"Okay, mimi sina la kusema, nyinyi ni watu wa usalama, fanyeni kazi yenu, ila tu mzingatie sheria na haki."

"Hakuna maneno, na hii sisi ni kazi yetu na tumekuwa tukiifanya kwa weledi mkubwa."

**Jerry alimshika ili asianguke. Akatoa leso yake na kumfuta machozi yaliyokuwa yakitiririka kama bomba la mvua.**

Vayajo alitoka nje akiwa amebadilisha nguo, tayari kwa safari ya kwenda Dar es Salaam kwa ajili ya kuisaidia polisi, uchunguzi na kutoa maelezo ya pesa alizowekewa kwenye akaunti yake.

Machozi yalikuwa yanamtoka. Aliona aibu kumtazama Jerry kwa sababu tayari alikuwa ameshajua siri yote ya kwa nini alitoroka siku ile ya harusi.

Ni bwana, ambaye alimzuzua kwa pesa aliyomuingizia kwenye akaunti yake ambayo leo imemletea matatizo. Na kabla ya hapo ilimpa tabu hata kumbembeleza Jerry ili amsamehe. Kweli fedha ni fedheha. Akakumbatiana na mama yake, wakalia wote kwa pamoja.

"Mwanangu umefanya nini sasa? Haya umeyatafuta mwenyewe. Kwa nini hukutulia tu ukaolewa? Haya angalia leo, yote uliyoyafanya yamekutokea puani. Ndoa hakuna na pesa hakuna. Umekosa mwana na maji ya moto." Alilia na kuomboleza mama Vayajo kwa kwikwi.

Ilibaki kidogo Jerry aende kuwaachanisha mtu na mama yake kwa sababu alivyokuwa akilia na kuomboleza ilimchoma sana moyoni. Lakini akakumbuka kuwa yeye ni 'mkwe', asingeweza kwenda kumshika mama Vayajo au mama Zulfa

Kama alivyokuwa anafikiria, kazi hiyo ilifanywa na mmoja wa maaskari kanzu waliokuja.

"Basi mama inatosha, tunachelewa sana, nakuomba usihuzunike sana, anaweza akarejea kama hahusiki. Tunachotaka sisi ni kwamba tujidhihirishe kama watuhumiwa tuliowakamata ni hao hao au kuna wengine ambao nao wapo kwenye huu mgao. Kama tutajidhihirishia ulikuwa ni sababu ya kuhongana, basi hatuna matatizo, tutamuachia." Alisema askari yule.

Kati ya wote waliokuwa wamsikiliza hakuna aliyemwelewa au kumuamini zaidi ya Jerry peke yake. Wote walidhani kuwa ile ni siasa tu ili wamchukue na kwenda kumfunga jela.

Jerry ndiye aliyefahamu kuwa kwa hali jinsi ilivyo ni kwamba Vayajo ataachiwa baada ya uchunguzi kwa sababu hawezi kuwa mwizi wala mtakatishaji pesa. Hiyo pesa iliingizwa kwa sababu za mapenzi tu na huyo jamaa ambazo zilimshawishi kutoroka ndoa, na askari kama wakidhihirisha hilo kwenye uchunguzi wao watamuachia. Kitu pekee ambacho hakujua ni kwamba atakaa kokoroni kwa muda gani hadi hapo uchunguzi utakapokamilika.

Vayajo hakumuaga Jerry kwa aibu, lakini pia mdogo wake Zulfa. Badala yake alimtupia jicho kali, huku akiwa mikononi mwa polisi kabla ya kuingizwa ndani ya gari.

Muda wote huo, Zulfa ni kama alikuwa amepigwa na butwaa na ilionekana kama hajui nini kinaendelea. Nadhani alichoona ni kama ndoto, au kitu ambacho anakishuhudia kwenye televisheni. Damu nzito kuliko maji, machozi yalianza kumtiririka kimya kimya bila kutoa sauti.

Wakati mama Vayajo akiendelea kulia akiwa anagaragara chini, Zulfa yeye alikuwa amejiegemeza kwenye mwili wa Jerry akitokwa machozi.

Jerry alimshika ili asianguke. Akatoa leso yake na kumfuta machozi yaliyokuwa yakitiririka kama bomba la mvua.

Wote waliokuwa hapo walienдelea kuitazama gari ya maaskari iliyombeba Vayajo ilianza kuondoka, ikiyoyoma kwenye barabara ya vumbi hadi ikatokomea kwenye upeo wa macho yao.

**MWISHO**



# ASLAY AGOMA KUMZUNGUMZIA ALI KIBA

MWANAMUZIKI wa kizazi kipya, Aslay amesema yupo sehemu sahihi, licha ya msanii mkongwe Ali Kiba kujiondoa lebo ya Rock Star Africa.

Muimbaji huyo ambaye tayari ameachia nyimbo tatu kwa mpigo baada ya ukimya wa muda mrefu, amesema anachofikiria kwa sasa ni kufanya mambo makubwa kwa ajili ya mashabiki wake na si vingine.

Aslay amesema kila msanii ana malengo yake binafsi, hivyo hawezi kuzungumza jambo lolote ambalo linamuhusu mwingine kwa hali yoyote.

# KWELI KAOLEWA?



NDOA ya mtoto wa msanii wa Bongo Muvi, Kajala Masanja, imezidi kuleta utata kiasi ambacho baadhi ya watu wanaamini jambo hilo limekuwa kama kiki kutokana na misukosuko aliyopitia mama yake.

Hivi karibuni kulisambaa picha ya Paula akionekana akivishwa pete na mtu anayedaiwa kuwa ni mume wake aliyetambuliwa kwa jina la Ally, lakini haijafahamika sehemu ilipofanyika harusi hiyo na wala tarehe husika.

Hata hivyo, kupitia ukurasa wake wa Facebook, aliyekuwa mpenzi wake, mwanamuziki wa Bongo Fleva, Rayvanny, alimtakia heri kwa kundika "Hongera sana P.. na iwe heri,"

Hata hivyo, Rayvanny hajaweza kutuliza wasiwasi wa watu wanaomfuatilia binti huyo, wengi waliendelea kurusha vijembe mitandaoni, wakiamini kinachoonekana siyo halisi.

Kinachowafanya wengi kutoamini kwamba kweli Paula ameolewa ni hatua ya kupakia picha bila ya kumuonyesha sura mume wake mpya, na pia hatua ya kutumia mstari wa kionjo cha wimbo wa Rayvanny kumtambulisha mpenzi huyo mpya kisemacho "mwamba huyu hapa"

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### LEWIS AWANIWA

KLABU za Leicester na Everton zinamfuatilia kiungo wa kati wa Bologna na Scotland, Lewis Ferguson mwenye umri wa miaka 23. ***(Nicolo Schira)***

### COOPER APAMBANIWA

KLABU ya Nottingham Forest inakabiliwa na upinzani mkali wa kutaka kumbakisha kocha Steve Cooper msimu ujao huku Klabu kadhaa za Ligi Kuu vikiwa vimevutiwa nae. ***(Mail)***

### DE GEAN NA MAN

MAZUNGUMZO yanaendelea kati ya Manchester United na David de Gea. Kipa huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 32, mkataba wake unamalizika msimu wa joto, lakini anatamani kusalia Old Trafford. ***(Fabrizio Romano)***

### GREENWOOD OFA MEZANI

MANCHESTER United wamepokea ofa kutoka kwa Klabu za nchini Uturuki kwa ajili ya mshambuliaji wao, Mason Greenwood mwenye umri wa miaka 21, ambaye bado amesimamishwa na klabu hiyo licha ya mashtaka ya ubakaji kufutwa mwezi uliopita. ***(Telegraph)***

### KHVICHA KUBAKISHWA

KLABU ya Napoli inabakia kuwa na uhakika wa kumbakisha winga wa Georgia, Khvicha Kvaratskhelia mwenye umri wa miaka 22, licha ya Manchester City, Chelsea, Real Madrid na Barcelona kumwindwa. ***(90min)***

### MANOR MKATABA WA KUDUMU

KLABU ya Fulham inataka kufanya uhamisho wa mkopo wa winga wa Israel, Manor Solomon mwenye umri wa miaka 23 kutoka Shakhtar Donetsk kuwa wa kudumu msimu huu. ***(Standard)***

### LEAO AWANIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain itakabiliana na ushindani kutoka kwa Liverpool kuwania saini ya mshambuliaji wa AC Milan na Ureno, Rafael Leao, huku klabu hiyo ya Merseyside ikiwa tayari kumjumuisha winga wa Colombia, Luis Diaz mwenye umri wa miaka 26, katika mkataba wa kubadilishana mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato)***

### XHAKA KUONGEZEWA

ARSENAL inafanya mazungumzo na kiungo wa kati wa Uswisi, Granit Xhaka, 30 kuhusu kuongezwa kwa mkataba mpya wa miaka miwili. ***(CaughtOffside)***

### SAVIC AWANIWA

KLABU za Arsenal, Newcastle United na West Ham zimetoa ofa ya karibu euro milioni 40 kumnunua kiungo wa kati wa Lazio na Serbia, Sergej Milinkovic-Savic, 27. ***(Calciomercato)***

### TIERNEY ATAKIWA

NEWCASTLE United inapanga kumnunua beki wa Arsenal na Scotland, Kieran Tierney mwenye umri wa miaka 25 wakati wa msimu wa joto. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# FIRMINO KUONDOKA

**LIVERPOOL,** England

**Ni mwishoni mwa msimu huu, baada ya miaka nane ya kukaa hapo Anfield...**

MSHAMBULIAJI wa Brazil, Roberto Firmino ataondoka Liverpool mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu.

**Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 amekuwa na Wekundu hao tangu ajiunge nao kwa mkataba wa pauni milioni 29 kutoka Hoffenheim, Juni 2015.**

Firmino ameisaidia Liverpool kushinda taji la Ligi ya mabingwa Ulaya, Ligi Kuu ya England, Kombe la FA, Kombe la EFL na Kombe la Klabu bingwa ya Dunia tangu alipotua hapo.

Ameichezea Liverpool mechi 353, akifunga mabao 107 na kutoa asisti 70.

Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp alikuwa amesema anataka Firmino abaki na klabu hiyo na, wakati mchezaji huyo alikuwa kwenye majadiliano kuhusu mkataba mpya, amechagua kuhama.

Muda wa kucheza wa Mbrazil huyo umekuwa mdogo hivi karibuni kutokana na majeraha ya misuli na kuwasili kwa Diogo Jota, Luis Diaz, Darwin Nunez na Cody Gakpo.

Firmino, ambaye anaheshimiwa sana na mashabiki wa Wekundu hao, alicheza katikati ya washambuliaji watatu wa Liverpool - akiongozwa na Mohamed Salah na Sadio Mane, ambaye aliihama klabu hiyo na kujiunga na Bayern Munich mwaka jana.

Kwa pamoja waliisaidia Liverpool kubeba taji lao la kwanza la ligi ya England katika kipindi cha miaka 30 waliposhinda msimu wa 2019-2020. Firmino amecheza mechi 26 katika mashindano yote msimu huu, akifunga mabao tisa na kutoa asisti nne.

Hakuitwa kwenye kikosi cha Brazil kilichoshiriki Kombe la Dunia mwaka jana nchini Qatar, huku timu hiyo ikitolewa hatua ya Robo fainali.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 499,

MECHI KALI
LIVERPOOL
VERSUS
MANCHESTER UTD
1 | 2.42
X | 3.38
2 | 2.62

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# NEYMAR, MARTINELLI WAACHWA BRAZIL




**RIO DE JANEIRO,** Brazil

NEYMAR, Gabriel Martinelli na Bruno Guimaraes ni miongoni mwa wachezaji nyota waliokosekana kwenye kikosi cha wachezaji 23 wa Brazil kitakachocheza mechi ya kirafiki nchini Morocco baadaye mwezi huu.


Neymar alifunga rekodi ya mabao ya Selecao hao ya muda wote ya marehemu Pele (77) kwa bao lake dhidi ya Croatia wakati Brazil ikitolewa katika robo fainali ya Kombe la Dunia, Desemba mwaka jana.

Jeraha la kifundo cha mguu alilopata katika ushindi wa hivi karibuni wa Paris Saint-Germain dhidi ya Lille litamfanya asiweze kucheza dhidi ya Morocco.

Huku kocha mkuu Tite akiachia ngazi baada ya kushindwa huko Qatar, kocha wa muda wa Brazil, Ramon Menezes ndiye atakayesimamia mechi hiyo ya kirafiki na amechagua wachezaji tisa wapya, akiwemo Andrey Santos wa Chelsea aliyerejea kwa mkopo Vasco da Gama - kiungo wa kati wa Wolves, Joao Gomes na mshambuliaji wa Athletico Paranaense, Vitor Roque.

Wachezaji wawili wa Manchester United, Casemiro na Antony wameungana na wengine wa Ligi Kuu, Ederson, Emerson Royal, Renan Lodi, Lucas Paqueta na Richarlison, huku akiwaacha wachezaji watatu wa Liverpool, Alisson, Fabinho na Roberto Firmino.

Brazil itacheza na Morocco waliofika nusu fainali kwenye Kombe la Dunia, Machi 25 katika Uwanja wa Ibn Batouta mjini Tangier.




## *Sergi asaini mkataba mpya*

**BARCELONA,** Hispania

NYOTA wa Barcelona, Sergi Roberto amesaini mkataba mpya wa mwaka mmoja na vinara hao wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 aliweka bayana kusaini mkataba wa miezi 12 na Barca Juni mwaka jana, baada ya kuhusishwa na uhamisho.

Na Roberto sasa atabakia na wababe hao wa Katalunya kwa angalau msimu mwingine baada ya klabu hiyo kuthibitisha Ijumaa kuwa wamefikia makubaliano ya mkataba mpya na atakaa hapo hadi Juni 2024.

Kifungu cha muda mrefu cha kumnunua Sergi kimebakia kuwa euro milioni 400.

Aliteuliwa kuwa mmoja wa manahodha wa kikosi cha kwanza cha Xavi alipoongeza mkataba wake mwaka jana na ameshiriki mara 14 kwenye ligi msimu huu.

Roberto alianza kuichezea Barca mwaka 2010 na amefanikiwa kuichezea klabu hiyo mechi 339.

# HABARI MICHEZO

,870,280

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/03/22 | 22:45 | Huddersfield vs Bristol City | 2.54 | 3.14 | 2.64 |
| 02. 07/03/22 | 22:45 | Walsall vs Bradford City | 2.54 | 2.88 | 2.78 |
| 03. 07/03/22 | 22:45 | Cheltenham vs Lincoln | 2.48 | 3.20 | 2.65 |
| 04. 07/03/22 | 23:00 | Plymouth vs Derby | 2.70 | 3.25 | 2.42 |
| 05. 08/03/22 | 01:00 | Audax Italiano vs Universidad Catolica | 2.95 | 3.01 | 2.33 |
| 06. 08/03/22 | 01:00 | Tacuary Asuncion vs Club General Caballero Jlm | 2.47 | 3.37 | 2.52 |
| 07. 08/03/22 | 13:00 | Shonan Bellmare vs Urawa Red Diamonds | 2.40 | 3.05 | 2.55 |
| 08. 08/03/22 | 13:00 | Vissel Kobe vs Nagoya Grampus | 2.22 | 3.15 | 3.00 |
| 09. 08/03/22 | 13:00 | Sagan Tosu vs Consadole Sapporo | 2.51 | 3.27 | 2.53 |
| 10. 08/03/22 | 13:00 | Kyoto Sanga vs Gamba Osaka | 2.29 | 3.20 | 2.84 |
| 11. 08/03/22 | 13:00 | Kashiwa Reysol vs Kashima Antlers | 2.75 | 3.32 | 2.30 |
| 12. 08/03/22 | 16:30 | Liptovsky Mikulas vs MFK Skalica | 2.55 | 3.15 | 2.55 |
| 13. 08/03/22 | 18:00 | Ismaily SC vs Farco FC | 2.50 | 2.71 | 3.16 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 05/03/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 1994 | SBV Excelsior vs Sparta Rotterdam | 3.19 | 3.33 | 2.10 |
| 15:00 | 2783 | Troyes vs Monaco | 5.53 | 4.45 | 1.47 |
| 16:00 | 5577 | Konyaspor vs Giresunspor | 1.84 | 3.58 | 3.79 |
| 16:00 | 5783 | Valladolid vs Espanyol | 2.37 | 3.19 | 2.99 |
| 16:30 | 2249 | FC Krasnodar vs Torpedo Moscow | 1.46 | 4.19 | 6.08 |
| 16:30 | 2927 | Waalwick vs PSV Eindhoven | 6.11 | 4.63 | 1.41 |
| 16:30 | 5033 | WSG Wattens vs LASK Linz | 3.28 | 3.39 | 1.96 |
| 17:00 | 1056 | Toulouse vs Clermont Foot | 1.75 | 3.66 | 4.15 |
| 17:00 | 1239 | Sudtirol vs Perugia | 2.66 | 2.97 | 2.66 |
| 17:00 | 1609 | Ternana vs Benevento | 2.48 | 3.14 | 2.72 |
| 17:00 | 2412 | Olympiakos vs Levadiakos | 1.17 | 6.38 | 15.94 |
| 17:00 | 3382 | Nottingham vs Everton | 2.55 | 2.94 | 2.79 |
| 17:00 | 4211 | Como vs Modena | 2.12 | 3.18 | 3.29 |
| 17:00 | 4391 | Montpellier vs Angers | 1.81 | 3.51 | 4.05 |
| 17:00 | 4498 | Brescia vs Cagliari | 2.78 | 2.98 | 2.53 |
| 17:00 | 4531 | NK Mura vs Maribor | 3.35 | 3.24 | 1.99 |
| 17:00 | 4831 | Ascoli vs Bari | 2.62 | 2.99 | 2.67 |
| 17:00 | 5034 | Strasbourg vs Brest | 1.98 | 3.20 | 3.74 |
| 17:00 | 5245 | Frosinone vs Venezia | 1.81 | 3.35 | 4.19 |
| 17:00 | 5280 | Spal vs Cittadella | 2.51 | 2.98 | 2.82 |
| 17:00 | 5426 | Reims vs AC Ajaccio | 1.59 | 3.71 | 5.34 |
| 17:00 | 5631 | Sampdoria vs Salernitana | 2.20 | 3.15 | 3.15 |
| 17:30 | 5975 | Bayer Leverkusen vs Hertha BSC | 1.51 | 4.15 | 5.34 |
| 18:00 | 1038 | Royal Antwerp vs Mechelen | 1.51 | 4.25 | 5.33 |
| 18:15 | 1848 | Albacete Balompie vs Sporting Gijon | 2.22 | 2.94 | 3.34 |
| 18:15 | 2205 | Barcelona vs Valencia | 1.51 | 4.15 | 6.02 |
| 18:30 | 3118 | FC Zurich vs Servette Geneva | 1.90 | 3.42 | 3.74 |
| 18:30 | 3201 | Gil Vicente vs Maritimo | 1.86 | 3.45 | 3.90 |
| 18:30 | 3763 | FC Sion vs FC Lugano | 2.73 | 3.41 | 2.35 |
| 18:45 | 5506 | Ajax vs NEC Nijmegen | 1.21 | 6.28 | 9.81 |
| 19:00 | 3301 | Rapid Vienna vs RB Salzburg | 3.55 | 3.40 | 1.87 |
| 19:00 | 3667 | Besiktas vs Ankaragucu | 1.54 | 4.14 | 5.14 |
| 19:05 | 3913 | Lyon vs Lorient | 1.50 | 4.24 | 5.52 |
| 19:30 | 4732 | Liverpool vs Manchester Utd | 2.42 | 3.38 | 2.62 |
| 19:30 | 5327 | VfL Wolfsburg vs Eintracht Frankfurt | 2.38 | 3.34 | 2.70 |
| 20:00 | 4847 | Inter vs Lecce | 1.32 | 4.72 | 8.45 |
| 20:30 | 1691 | Malaga vs Racing Santander | 2.20 | 2.99 | 3.33 |
| 20:30 | 3135 | Lugo vs Zaragoza | 3.34 | 2.94 | 2.22 |
| 20:30 | 4206 | Rayo Vallecano vs Athletic Bilbao | 2.89 | 3.04 | 2.54 |
| 20:30 | 4818 | OFI Crete vs AEK Athens | 8.29 | 4.04 | 1.41 |
| 20:30 | 5043 | Copenhagen vs Odense | 1.44 | 4.37 | 6.56 |
| 21:00 | 1231 | Santa Clara vs Vitoria Guimaraes | 2.91 | 3.01 | 2.45 |
| 21:15 | 3979 | Union Saint Gilloise vs Eupen | 1.25 | 5.51 | 9.65 |
| 21:30 | 1496 | PAOK vs Ionikos Nikea FC | 1.24 | 5.09 | 13.79 |
| 22:00 | 4086 | Cambuur vs GO Ahead Eagles | 2.74 | 3.18 | 2.44 |
| 22:45 | 3047 | Rennes vs Marseille | 2.66 | 3.45 | 2.38 |
| 22:45 | 5721 | Roma vs Juventus | 2.55 | 2.94 | 2.79 |
| 23:00 | 1490 | Betis vs Real Madrid | 4.30 | 3.58 | 1.79 |
| 23:00 | 2916 | Ponferradina vs FC Cartagena | 2.55 | 2.99 | 2.75 |
| 23:30 | 4683 | Sporting Braga vs Rio Ave | 1.40 | 4.33 | 7.27 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



## TOWN CLASSIC YAAMUA KUANGUSHA MOJA MOJA

**Na Sabato Kasika**

BENDI mpya ya muziki wa dansi ya Town Classic, imefikisha nyimbo nne, huku ikiwa imekamilisha kurekodi mbili, katika mwendelezo wake wa kuandaa albamu ya kwanza.

**Meneja wa bendi hiyo Andrew Sekidia alitaja nyimbo hizo kuwa ni Shem Darling, No Stress, Ngayo na Acha Umbea, ambazo huporomoshwa katika bonanza la kila Jumapili, ndani ya ukumbi wa Msasani Beach Dar es Salaam.**

"Shem Darling na No Stress zimesharekodiwa na sasa tunajiandaa kurekodi hizo nyingine mbali, ukiwa ni mwendelezo wa kukamilisha albamu yetu ya kwanza ambayo inasubiriwa kwa hamu na mashabiki wetu," alisema Sekidia.

Aidha, alisema wakati huu ambao wanaendelea kuandaa nyimbo mpya, wamekuwa pia wakiboresha bonanza lao ili liwe na kuvutia zaidi na kupata wahudhuriaji wengi wanaofika kushuhudia bendi hiyo ikifanya vitu vyake.

"Tulianza bonanza mwishoni mwa Januari, lakini sasa tunaendelea kuliboresha kwa kuongeza vikundi vya burudani vikiwamo vya maigizo na sarakasi ili wanaofika wapate burudani ya kutosha.

Alisema bendi hiyo imepania kurudisha muziki wa dansi kwenye chati yake na kwamba njia mojawapo wanazotumia ili lengo hilo litimie, ni kuandaa nyimbo bila kuwa na haraka na pia kuwa na bonanza.

"Kwa kawaida bonanza huvuta mashabiki wengi, hivyo nasi tumeona kuna umuhimu wa kulianzisha na kuweka burudani mbalimbali ambazo zitahusisha vikundi mbalimbali vya burudani ambavyo huvuta watu wengi," alisema.

Bendi hiyo ilianza kutoa burudani mwishoni mwa mwaka jana, ambapo imekuwa ikifanya vitu vyake, katika kumbi mbalimbali kila mwisho wa wiki, huku ikimalizia na bonanza la Jumapili ndani ya Msasani Beach Club.

## Kocha mpya wa Taifa Stars huyu hapa

INATOKA UK. 24

makocha wengi bora barani Afrika na ana uzoefu mkubwa katika soka la vijana, kazi aliyoifanya kwa zaidi ya miaka 10 nchini Algeria na Ubelgiji.

Kocha Amrouche anayezungumza lugha za Kiarabu, Kifaransa, Kingereza na Kiswahili, kwa nyakati tofauti, amewahi kuwa Mkurugenzi wa Ufundi na Michezo katika klabu za Ubelgiji na Ukraine.

Ni Kocha mwenye Uefa Pro Licence na Shahada ya Uzamili katika kuwasoma watu na Utimamu (Mas- ters in Ergonomics in Physical Activity).

Amrouche amekuwa akifanya kazi za ukufunzi pia kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF) katika kuzalisha walimu wa soka.

Katika wakati wote wa Mkataba wake Amrouche atalipwa mshahara na Serikali.



Getrude Dyabene (kushoto) kutoka kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) na Mbunge wa vitu maalumu kutoka Mkoa wa Pwani, Hawa Mchafu na wanawake wengine wakicheza muziki kwenye Uwanja wa Mwanakalenge Bagamoyo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake duniani yaliyoandaliwa na kituo hicho. **PICHA: SABATO KASIKA**

## *Simba kazi moja kwa Vipers*

INATOKA UK. 24

bu Vipers anawajua wana wachezaji wazuri sana mbele na wenye kasi, hivyo wanatakiwa kucheza kwa makini na utulivu mkubwa ili wasifanye makosa ambayo yanaweza kuwagharimu.

Kocha huyo alisema wanatakiwa kushinda ili kuwapa furaha mashabiki wao ambao wamekuwa wakiwasapoti na kwenda kila sehemu wanapokwenda .

Simba leo inaendelea na kampeni yao ya hamasa kuelekea mchezo huo kwa safari hii kuja tofauti na watakuwa katika ufukwe wa Coco 'Wenye nchi Beach Party'.

Hamasa hiyo inaanza saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni ambapo kutakuwa na burudani mbalimbali huku kispika kikiwepo kuwapa burudani na kuhamasisha wanasimba kununua tiketi mapema ili kujitokeza kwa wingi uwanjani.

# Michezo

Jumapili Machi 5, 2023

Nipashe




**Firmino kuondoka Liverpool**

UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakiwa mazoezini. **PICHA: SIMBA**

## Kocha mpya Taifa Stars huyu hapa

**Na Adam Fungamwango**

SHIRIKISHO la soka Tanzania (TFF) limemtangaza Adel Amrouche mwenye umri wa miaka 58 kuwa kocha mkuu wa timu ya Taifa, Taifa Stars.

Amrouche raia wa Ubelgiji mwenye asili ya Algeria ana uzoefu mkubwa na soka la Afrika baada ya kufundisha klabu na timu za taifa katika ukanda wa Kusini, Mashariki, Kati na Kaskazini.

Amewahi kuwa Kocha Bora wa Afrika Mashariki mwaka 2013 wakati akiinoa na kuipa Kenya, Harambee Stars, ubingwa wa Cecafa Challenge na kabla alifika nusu fainali mara mbili akiwa na Burundi.

Akiwa na Harambee Stars aliweka rekodi ya kucheza michezo 20 bila kupoteza.

Kocha Amrouche amewahi pia kuzinoa timu za taifa za Equatorial Guinea, Botswana, Libya na Yemen kwa nyakati tofauti.

Akiinoa DC Motema Pembe aliiwezesha kufanya vizuri katika michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho akiwa ameipa mara mbili ubingwa wa Ligi Kuu ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), DRC Super Cup.

Uzoefu mwingine kwa klabu, amezifundisha RC Kouba, USM Alger, alizowahi kuzichezea na MC Algiers, zote za Algeria.

Aidha, Kocha Adel ni mkufunzi wa walimu wa Pro Licence wa Shirikisho la Soka Ulaya (UEFA) akizalisha

INAENDELEA UK. 23

# Simba kazi moja tu kwa Vipers

### ●●● Kocha ataka umakini mkubwa kwa wachezaji ili kupata ushindi na kujihakikishia...

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', amewataka wachezaji wake kuwa makini katika mechi yao ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Vipers ya Uganda na kuhakikisha wanaibuka na ushindi.

Mbrazili huyo alisema hayo akijua kwamba ushindi pekee ndio utakaowapa Wekundu hao wa Msimbazi mwanga wa kwenda hatua ya robo fainali katika mchezo huo utakaochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Robertinho alisema mchezo huo muhimu sana kwao hasa kucheza nyumbani kwa kupata matokeo mazuri ya ushindi na ili yasitokee kama ilivyokuwa mechi yao ya kwanza dhidi ya Raja Casablanca.**

Alisema wanahitaji sana ushindi dhidi ya Vipers kwa sababu ya kufikia malengo yao ya kuvuna alama tatu za nyumbani na kupata pointi hizo lazima wachezaji wake kuwa makini na kupambana.

"Tunahitaji ushindi kwenye mechi hii, ushindi ambao utazidi kutusogeza mbele kwenye harakati zetu za kucheza robo fainali. Tunatakiwa kushinda michezo yote bila kumuangalia mpinzani wetu," alisema Robertinho.

Alisema, ni mchezo mgumu, kwa saba-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >